Sehemu ya 4
Australia leo

Australia ni mojawapo ya nchi kubwa zaidi ulimwenguni.

Ni nchi ya sita kubwa zaidi ulimwenguni.

Australia leo

Katika kurasa hizi utajifunza kuhusu kile kinachofanya nchi hii iwe maalum sana. Utajua zaidi juu ya utamaduni wetu, wavumbuzi wetu na utambulisho wetu wa kitaifa. Duniani leo, Australia ni mbia mkuu wa biashara na uuzaji na ni raia wa ulimwengu anayeheshimiwa. Tunathamini wahamiaji wapya kwa kukua na kubadilika kwa nchi yetu.

Nchi

Australia ni ya kipekee kwa njia nyingi. Kati ya bara saba za ulimwengu, Australia ndiyo pekee ambayo inakaliwa na taifa moja. Tuna idadi ndogo zaidi duniani, iliyo na watu wawili kwa kila kilomita za mraba.

Australia ni mojawapo ya nchi kubwa mzee zaidi ulimwenguni. Ni nchi ya sita kubwa zaidi ulimwenguni. Pia ndilo bara kavu zaidi, kwa hivyo katika sehemu nyingi za Australia, maji ni rasilimali muhimu sana.

Nyingi za nchi ina mchanga bovu, ulio na asilimia 6 inayofaa kwa ukulima. Nchi kavu za ndani huitwa ‘porini’. Kuna heshima kuu kwa watu wanaoishi na kufanya kazi katika mazingira haya ya mashambani na magumu. Wengi wao wamekuwa sehemu ya hadithi za jadi Australia.

Kwa sababu Australia ni nchi kubwa sana, hali ya anga hubadilika katika sehemu tofauti za bara. Kuna maeneo ya joto huko kaskazini Australia na jangwa katikati.

Kusini ndani, hali joto zinaweza kubadilika kutoka msimu wa baridi ulio na theluji ya milima, kuwa mawimbi ya joto katika msimu wa joto.

Kwa kuongezea majimbo sita na wilaya mbili za nchi ya ndani, Serikali ya Australia pia husimamia, kama wilaya, Visiwa vya Ashmore na Cartier, Kisiwa cha Krismasi, Visiwa vya Cocos (Keeling), Wilaya ya Jervis Bay, Visiwa vya Coral Sea, Kisiwa cha Heard na Visiwa vya McDonald katika Wilaya ya Antarctic ya Australia, na Kisiwa cha Norfolk.

Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

Zaidi ya asilimia 11 ya nchi yetu imelindwa na nchi ya asili, hifadhi au mbuga la kitaifa ambalo huendeshwa kwa utunzaji kwa viwango vya kimataifa. Maeneo kumi na saba ya Australia yameorodheshwa kwenye orodha ya Urithi wa Ulimwengu wa Shirika la Kielimu, Kisayansi na Kitamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.

Maeneo ya Visukuku vya Wanyama huko Australia Kusini na Queensland



Misitu ya mvua ya Gondwana ya New South Wales na Queensland

Mbuga la Kitaifa la Kakadu katika Wilaya ya Kaskazini

Kisiwa cha Fraser mbali na pwani la Queensland kusini

Great Barrier Reef huko Queensland

Kisiwa cha Lord Howe mbali na pwani ya New South Wales

Milima ya Greater Blue magharibi mwa Sydney

Kisiwa cha Heard na Visiwa vya McDonald katika Wilaya ya Antarctic ya Australia

Kisiwa cha Macquarie kusini mwa Tasmania

Mbuga la Kitaifa la Purnululu Magharibi mwa Australia

Jumba la Sydney Opera

Maeneo yenye Umaji ya Queensland

Jumba la Maonyesho ya Kifalme na Bustani za Carlton Melbourne

Nyika yaTasmanian

Willandra Lakes huko New South Wales

Shark Bay huko Western Australia

Mbuga la Kitaifa la Uluru-Kata Tjuta katika Wilaya ya Kaskazini

Tunakuhimiza kupanua uzoefu wako wa Australia kwa kutembelea maeneo haya ya ajabu na zaidi. Unaweza kutembea nyikani au ufuoni, milimani au kwenye misitu ya mvua. Kila hatua unayochukua iko karibu zaidi kujiungana na nchi hii kubwa na yenye nguvu.

Nchi kubwa

Ukubwa wa Australia umeongeza uvumbuzi na uzinduzi.

Siku za mapema, watu katika pori nyakati zingine walilasimika kusafiri kwa siku kadhaa kutembelea daktari aliye karibu. Watoto wengi porini waliishi mbali sana kuenda shule yoyote ya kawaida.

Familia za porini zilipata ugumu wa kutengwa. Vituo kubwa vya ng'ombe zingeweza kuwa maelfu ya kilomita za miraba kwa saizi. Wanawake na watoto ambao walikaa huko wanaweza kukosa kuona mtu mwingine kwa miezi. Hakukuwa na simu na watu walihisi wametengwa na kuogopa.

Haya yalikuwa matatizo ambayo Waaustralia wakuu walitatua kupitia uzinduzi na uvumbuzi.

Redio ya pedali

Mnamo 1929, Alfred Traegar, kutoka Adelide, alipanga redio ya kwanza iliyoendeshwa na pedali. Watumiaji wangeweza kuweka redio ya njia mbili kwa kusukuma pedali kwa miguu yao. Nyumba pweke, vituo vya misheni mashambani na jamii za watu wa asili zote zilifaidika kutoka kwa uvumbuzi huu. Wanawake waliotengwa sasa walipata marafiki kupitia mitabendi.

Redio ya pedali ilisaidia kuanzisha taasisi mbili kubwa za Australia, Royal Flying Doctor Service na Shule ya Angani (School of the Air).

Huduma ya Kifalme ya Daktari wa Ndege (Royal Flying Doctor Service)

Reverend John Flynn aliishi na kufanya kazi na watu wa jamii za mashambani. Wazo lake lilikuwa kuleta daktari kwa mgonjwa porini haraka iwezekanavyo, kwa kutumia ndege. Alipokea msaada kutoka kwa serikali, shirika la ndege la Qantas na misaada ya wafadhili. Huduma ya Kifalme ya Daktari wa Ndege ilianza mnamo 1928 lakini kulikuwa na watu katika sehemu za mashambani ambao hawakuweza kupigia huduma simu. Utangulizi wa redio ya pedali ilihakikisha watu walio kwenye vituo vya mbali wangeweza kuita daktari haraka iwezekanavyo.

Shule ya Angani

Hadi 1950, watoto walioishi katika sehemu zilziotengwa walilazimika kwenda shule za mabweni au kukamilisha masomo yao kwa kupitia barua.

Adelaide Miethke, Makamu wa Rais wa Huduma ya Kifalme ya Daktari wa Ndege huko Australia Kusini, aligundua kwamba huduma ya redio ya Flying Doctor ingeweza pia kusaidia watoto nyumbani kuzungumza na waalimu wao. Huduma ya Alice Springs ilianza kupeperusha masomo hayo kwa redio ya njia mbili mnamo 1948. Shule ya Angani (School of the Air) ilianzishwa rasmi miaka michache baadaye. Shule ya Angani Australia (School of the Air) pia ilisaidia nchi zingine kuanza mipango yao kama hiyo.

Redio mzee ya pedali sasa imebadilishwa na vipokea masafa ya juu, lakini Huduma ya Kifalme ya Daktari wa Ndege ya Australia na Shule ya Angani (School of the Air) inaendelea kuhudumia na kufaidi watu katika jamii za mashambani huko Australia.

Watoto wanaosoma kupitia Shule ya angani (School of the Air) huko New South Wales

Utambulisho wa Australia

Utambulisho wa Australia kimeundwa na urithi wetu wa kipekee, utamaduni na desturi ya hodari ya watu wetu.

Michezo na burudani

Waaustralia wengi wanapenda michezo na wamepata matokeo ya kupendeza katika kiwango cha kimataifa.

Tunajivunia sifa yetu kama taifa la 'wachezaji wazuri'. Wachezaji wa Australia wanatamanika kama mabalozi kwa thamani ya bidii, haki sawa na kufanya kazi kama timu.

Kote katika historia, michezo imetambua watu wa Australia na imetuunganisha. Kuanzia makazi ya mapema, michezo imetoa njia ya kutoroka kutoka kwa ukweli wa maisha magumu. Hata wakati wa vita, wanachama wa Jeshi la Ulinzi la Australia (Australian Defence Force) ilipanga mashindano ya michezo kusaidia kupunguza mafadhaiko ya uwanja wa vita.

Michezo pia hutoa mwafaka ambao huruhusu wachezaji wote na watazamaji kuhisi kujumuishwa na sehemu ya kitu ambacho ni muhimu kwa jamii ya Australia.

Waaustralia wengi hushiriki katika michezo za timu. Nembo za kriketi, mpira wa kikapu, netibali, mpira wa magongo na kandanda ziko kati ya zile zinazojulikana zaidi.

Kupiga dimbwi, tenisi, riadha, gofu na uendeshaji baisikeli ni burudani zinazojulikana zaidi. Pia ni michezi ambayo Waaustralia hufanya bora kabisa katika mashindano ya kimataifa. Shughuli zingine zinzojulikana ni pamoja na kutembea msituni, kutekeleza katika mawimbi mweupe na kuteleza katika theluji kwa skii.

Waaustralia pia hucheza na hupenda kutazama kandanda (pia inajulikana kama soka), ligi ya raga, umoja wa raga na Sheria za kandanda ya Australia. 'Sheria za Aussie' ni mchezo wa kipekee wa Australia.

Australia haswa inajivunia mafanikio yake ya kimataifa kwenye mchezo wa kriketi. Timu za Australia na Kiingereza zinachuki kali tangu karne ya 19.

Kombe la Melborne, 'mbio ambayo hukomesha taifa', ni mojawapo ya mbio za farasi tajiri sana na zenye changamoto zaidi ulimwenguni. Kombe la kwanza la Melbourne lilifanyika mnamo mwaka wa 1861. Jumanne ya kwanza ya Novemba, Siku ya Kombe la Melbourne, imekuwa sikukuu ya umma katika Victoria tangu 1877.

Mshindi wa dhahabu mara tano kwa Olimpiki, Ian Thorpe

Mwanachama wa timu ya Kandanda ya Kitaifa ya Wanawake ya Australia

Sir Donald Bradman (1908 – 2001)

Sir Donald Bradman ndiye mchezaji bora wa kriketi wa nyakati zote na ndiye shujaa wa michezo ya Australia.

Alilelewa Bowral, New South Wales, Donald Bradman alicheza mchezo wa kwanza wa kriketi ya Australia mnamo 1928.

Alikuwa mdogo lakini alikuwa na mbio miguuni mwake. Katika safari yake ya kwanza huko Uingereza mnamo 1930, alivunja karibu rekodi zote za kushindana. Alipofika umri wa 21, alikuwa tayari shujaa wa Australia.

Kwenye safari yake ya mwisho mnamo 1948, timu take ilijulikana kama 'The Invincibles'; kwani hawakushindwa hata mechi moja walizocheza dhidi ya Uingereza.

Sir Donald Bradman, anajulikana kama 'The Don', anatambulika kama mchezaji bora ulimwenguni. Kadiri yake ya kushindana ilikuwa 99.94.

Sanaa

Australia ina sanaa za nguvu ambazo ni pamoja na mila za utamaduni wa watu wa asili na mchangayiko mkubwa wa tamaduni za wahamiaji. Aina zote za sanaa za kutumbuiza za kutazama, pamoja na filamu, mchezo wa sanaa, muziki na densi, huvutia hapa na ngambo.

Fasihi

Australia ina utamaduni wa nguvu wa fasihi ambao ulianza na kuhadithia kwa watu wa asili ya Australia na iliendelea na hadithi za kusimulia za wafungwa waliowasili mnamo karne ya 18.

Uandishi wa mapema wa Australia ni juu ya pori na ugumu wa maisha kama mazingira magumu. Waandishi kama Henry Lawson na Miles Franklin waliandika mashairi na hadithi juu ya pori na njia ya maisha ya Australia.

Mwandishi wa riwaya wa Australia, Patrick White, alipokea Tuzo la Amani la Nobel katika fasihi mnamo 1973. Waandishi wengine wa riwaya wanaojulikana wa kisasa wa Australia ni pamoja na Peter Carey, Colleen McCullough na Tim Winton.

Judith Wright (1915 – 2000)

Judith Wright alikuwa mshairi wa kipekee, mhifadhi na mfanya kampeni wa haki za watu wa asilia.

Ni mmoja wa washairi wanaopendwa zaidi Australia. Alielezea upendo wake kwa Australia na watu wake katika ushairi. Alituzwa tuzo nyingi pamoja na Tuzo la Encyclopaedia Britannica na Dhahabu ya Malkia (Queen's Gold Medal) kwa Ushairi. Alikuwa mwanachama wa Kamati ya Uhifadhi ya Australia (Australian Conservation Committee) na Kamati ya Mastakabathi ya watu wa asili (Aboriginal Treaty Committee).

Judith Wright anakumbukwa kwa ustadi wake kama mshairi na kuendeleza fasihi ya Australia na mabadiliko ya jamii na mazingira.

Sanaa na filamu

Michezo ya kuigiza ya Australia, filamu na watengenezaji filamu wanatambulika na kupendwa hapa na ng'ambo. Waigizaji wa Australia kama vile Cate Blanchett na Geoffrey Rush, na watengenezaji filamu kama Peter Weir wameshinda tuzo nyingi za kimataifa kwa ubora wao katika filamu.

Sanaa

Kazi za sanaa zinazotambulika zaidi ni michoro ya ikoni ya asili na mandhari ya msitu ya karne ya 19 kama vile Tom Roberts, Frederick McCubbin na Arthur Streeton. Kati karne ya 20, wasanii Russell Drysdale na Sidney Nolan walionyesha ugumu wa pori kutumia rangi wazi. Karibu zaidi, Brett Whiteley amesifiwa kimataifa kwa mtindo wake wa kipekee na wazi.

Muziki na densi

Waaustralia wamekumbatia na kufanikiwa katika kila eneo la muziki na wanatambulika kimataifa kwa michango yao ya muziki wa jadi, country na rock. Sauti ya Australia inayotambulika zaidi ni ile ya didgeridoo, chombo cha kucheza cha zamani cha watu wa asili.

Densi ya Australia imefana kwa sababu ya bidii ya wachezaji wakuu na mtaalam wa koreografia kama vile Sir Robert Helpmann, Meryl Tankard na Stephen Page.

Mafanikio na uvumbuzi wa Kisayansi

Waaustralia wana rekodi ya nguvu ya mafanikio na maendeleo ya kisayansi katika nyuga za matibabu, teknolojia, ukulima, uchimbuzi na utengenezaji.

Waaustralia kumi wametuzwa Tuzo la Amani la Nobel kwa uvumbuzi wa kisayansi na kimatibabu.

Wafanisi wa kisayansi pia wamepokea Tuzo la Mwaustralia wa Mwaka. Mnamo 2005, tuzo lilimwendea Professor Fiona Wood, ambaye alianzisha marashi ya ngozi kwa wahasiriwa wa kuungua. Mnamo 2006, tuzo lilimwendea Professor Ian Frazer, ambaye alianzisha chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi. Mnamo 2007, Professor Tim Flannery, mwanasayansi anayeongoza wa mazingira, alipokea tuzo.

Professor Wood na Professor Frazer wote walihamia Australia kutoka Briteni. Professor Frazer mvumbuzi mwenzi wa marehemu alikuwa Dr Jian Zhou, ambaye alihamia Uchina na pia akawa raia wa Australia.

Kondakta na raia wa hivi karibuni Vladimir Verbitsky na Western Australian Symphony Orchestra

Professor Fred Hollows (1929 – 1993)

Professor Fred Hollows alikuwa mtaalam wa ugonjwa wa macho (daktari wa macho) wa mapenzi makali ambaye alisaidia kurudisha kuona kwa watu zaidi ya milioni moja huko Australia na nchi zinazoendelea.

Fred Hollows alizaliwa huko New Zealand. Mnamo 1965, alihamia Australia na baadaye akawa kiongozi wa Idara ya Macho kwenye hospitali ya Sydney.

Aliamini sana usawa wa watu wote na alisaidia kuunda Huduma ya Matibabu ya kwanza ya Watu wa asili. Sasa kuna 60 kote Australia.

Kufikia 1980, Fred Hollows alikuwa anasafiri kote ulimwenguni kusaidia kuanzisha mipango ya afya katika nchi zinazoendelea. Alikuwa raia wa Australia mnamo Aprili 1989.

Kazi nzuri ya Professor Hollows inaendelea maishani mwake yote kupitia mke wake, na The Fred Hollows Foundation.

Waaustralia wa Mwaka

Kuanzia 1960, Tuzo la Mwaaustralia wa Mwaka amesherehekea mafanikio na mchango wa Waaustralia wanaoongoza. Mtu yeyote anaweza kuteua Mwaaustralia kutoka sehemu yoyote ya maisha kwa tuzo. Waaustralia wa Mwaka ni watu ambao wamefanikiwa katika kazi yao na wametumikia taifa.

2009 Professor Michael Dodson AM
Kiongozi wa asili

2008 Lee Kernaghan OAM
Mwimbaji, Mwanamuziki na Mwanzilishi wa ' Pass the Hat Around' Tours

2007 Professor Tim Flannery
Mwanasayansi, Mwandishi na Mhifadhi

2006 Professor Ian Frazer
Mtaalamu wa Kinga katika Kliniki

2005 Professor Fiona Wood AM
Mtaalam wa Upasuaji wa Ngozi na Kuungua

2004 Steve Waugh
Kapteni wa Jaribio la Kriketi na Mhisani

2003 Professor Fiona Stanley AC
Daktari wa watoto na magonjwa ya mlipuko

2002 Patrick Rafter
Bingwa wa Tenisi Amerika na Mwanzilishi wa Mfuko wa Fedha wa Cherish the Children

2001 Lt General Peter Cosgrove AC MC
Mkuu wa Jeshi la Australia 2000-2002

2000 Sir Gustav Nossal AC CBE FAA FRS
Mwanabaiolijia mtafiti

1999 Mark Taylor
Kapteni wa Jaribio la Kriketi

1998 Cathy Freeman
Bingwa wa Dunia na Riadha ya Olimpiki na Balozi wa Asili

1997 Professor Peter Doherty
Mshindi wa tuzo la Nobel katika Matibabu

1996 Doctor John Yu AM
Daktari wa watoto

1995 Arthur Boyd AC OBE
Msanii

1994 Ian Kiernan OAM
Mfanya kampeni ya 'Safisha Australia'

1992 Mandawuy Yunupingu
Kiongozi wa asili

1991 Archbishop Peter Hollingworth AO OBE
Wakili wa Haki ya Jamii

1990 Professor Fred Hollows AC
Daktari wa ugonjwa wa macho

1989 Allan Border AO
Kapteni wa Jaribio la Kriketi

1988 Kay Cottee AO
Mvunja rekodi wa Mwanamke pekee wa Yoti

1987 John Farnham
Mwimbaji na Mwanamuziki

1986 Dick Smith
Mpenda vituko na Mfadhili

1985 Paul Hogan AM
Mwigizaji

1984 Lowitja O'Donoghue CBE AM
Kiongozi wa asili

1983 Robert de Castella MBE
Bingwa wa Ulimwengu wa Mbio za Masafa

1982 Sir Edward Williams KCMG KBE
Kamishena,
Tume ya Australia ya Kifalme ya Uchunguzi wa Madawa

1981 Sir John Crawford AC CBE
Msanifu mjengo wa Ukuaji wa Australia Baada ya Vita

1980 Manning Clark AC
Mwanahistoria

Mafanikio yao hutufanya tufikirie juu ya ni nini zaidi tunaweza kuchangia kwa nchi nzuri zetu. Tuzo sasa ni pamoja na Mwaustralia mdogo wa Mwaka, Mwaustralia Mkubwa wa Mwaka na Shujaa wa Eneo wa Australia.

1979* Senator Neville Bonner AO
Seneta wa Kwanza wa watu wa asili

1979* Harry Butler CBE
Mhifadhi na Mwanaviumbe

1978* Alan Bond
Mwanabiashara

1978* Galarrwuy Yunupingu AM
Kiongozi wa asili

1977* Sir Murray Tyrrell KCVO CBE
Katibu wa Ofisi ya Gavana Mkuu

1977* Dame Raigh Roe DBE
Kiongozi wa Shirika la Wanawake wa Nchi (Country Women's Association)

1976 Sir Edward 'Weary' Dunlop AC CMG OBE
Mtaalam wa upasuaji wa Jeshi

1975* Sir John Cornforth AC CBE
Mshindi wa tuzo la Nobel katika Kemia

1975* Major General Alan Stretton AO CBE
Kamanda wa Oparesheni ya Msaada wa Darwin baada ya Cyclone Tracy

1974 Sir Bernard Heinze AC
Kondakta na Mwanamuziki

1973 Patrick White
Mshindi wa tuzo la Nobel katika Fasihi

1972 Shane Gould MBE
Bingwa wa Olimpiki wa Kuogelea

1971 Evonne Goolagong Cawley AO MBE
Bingwa wa Tenisi wa Wimbledon na Ufaransa

1970 His Eminence Cardinal Sir Norman Gilroy KBE
Mkadinali wa kwanza kuzaliwa Australia

1969 The Rt Hon Richard Gardiner Casey Baron of Berwick, Victoria and of the City of Westminister KG GCMG CH
Gavana Mkuu wa Australia 1956-69

1968 Lionel Rose MBE
Bingwa wa Dunia wa Dondi

1967 The Seekers
Kundi la Muziki

1966 Sir Jack Brabham OBE
Bingwa wa Mashindano ya Gari Duniani

1965 Sir Robert Helpmann CBE
Mwigizaji, Mchezaji, Mtungaji na Mtalaamu wa Koreografia

1964 Dawn Fraser MBE
Bingwa wa Olimpiki wa Kuogelea

1963 Sir John Eccles AC
Mshindi wa tuzo la Nobel katika Matibabu

1962 Alexander 'Jock' Sturrock MBE
Mrukaji wa Ubingwa wa Kombe la Amerika

1961 Dame Joan Sutherland OM AC DBE
Soprano

1960 Sir MacFarlane Burnet OM AK KBE
Mshindi wa tuzo la Nobel katika Matibabu

*Kati ya 1975 na 1979 Siku ya Baraza la Canberra Australia pia hutambulika kama Mwaustralia wa Mwaka.

Watu walioteuliwa awali baada ya jina la wapokeaji wa tuzo walikuwa wakati tuzo zilipokewa.

Pesa ya Australia

Pesa yetu inaonyesha watu na ikoni ambazo ni muhimu kwa Australia. Waaustralia wanaojulikana walioteuliwa kuonekana kwenye pesa ni watu ambao wameonyesha uzinduzi na kipawa kuu katika maeneo ya mabadiliko ya kijamii, kisayansi, kisiasa, mafanikio ya kijeshi na sanaa.

Jumba Mzee na Mpya la Bunge

Noti ya $5 inaonyesha Jumba Mzee na Mpya la Bunge huko Canberra.

Queen Elizabeth II (alizaliwa 1926)

Malkia Elizabeth II ni Mkuu wa Nchi ya Australia. Yeye ndiye Malkia wa Australia na Uingereza na huishi Uingereza. Amekuwa uwepo wa nguvu, thabiti wakati wote wa uongozi wake wa muda mrefu.

Dame Mary Gilmore (1865 – 1962)

Dame Mary Gilmore alikuwa mwandishi, mwanahabari, mshairi na mfanya kampeni wa mabadiliko ya kijamii. Yeye hukumbukwa kwa uandishi wake na kuzungumza kwa hisani ya wanawake, Waaustralia asili na maskini.

AB 'Banjo' Paterson (1864 – 1941)

Andrew Barton Paterson alikuwa mshairi, mwandishi wa nyimbo na mwanahabari. Aliandika chini ya jina la 'Banjo' Paterson na anakumbukwa kwa 'Waltzing Matilda', wimbo wa kitamaduni unaojulikana zaidi Australia.

Reverend John Flynn (1880 – 1951)

Mchungaji John Flynn alianza huduma ya kwanza ya matibabu wa hewa, Huduma ya Kifalme ya Daktari wa Ndege ya Australia. Anakumbukwa kwa kuokoa maisha mengi kwa kuleta huduma ya afya kwa maeneo ya mashambani ya Australia.

Mary Reibey (1777 – 1855)

Mary Reibey alikuwa mwanabiashara mwanamke mwanzilishi katika koloni ya New South Wales. Baada ya kuwasili Australia kama mfungwa kijana, alikuwa kiongozi wa kuheshimiwa katika jamii.

Edith Cowan (1861 – 1932)

Edith Cowan alikuwa mfanyikazi wa jamii, mwanasiasa na mtetezi wa wanawake. Alikuwa mwanamke wa kwanza kuteuliwa na bunge la Australia.

David Unaipon (1872 – 1967)

David Unaipon alikuwa mwandishi, mzungumzaji wa umma na mzinduzi. Anakumbukwa kwa mchango wake kwa sayansi na fasihi, na kwa kuboresha hali za watu wa asilia.

Sir John Monash (1865 – 1931)

Sir John Monash alikuwa mhandisi, msimamizi na mmoja wa kamanda wakuu wa jeshi la Australia. Anakumbukwa kwa uongozi wake, maarifa na ufasaha wa lugha.

Dame Nellie Melba (1861 – 1931)

Dame Nellie Melba alikuwa soprano maarufu ulimwenguni. Anajulikana kote ulimwenguni kama ‘Malkia wa Nyimbo’, alikuwa mwimbaji wa Australia wa kwanza kutambulika kimataifa.

Siku na sherehe za kitaifa

Siku kuu za kitaifa za Australia huonyesha urithi wetu wa Yahudi-Kikristo na husherehekea hatua ambazo zimeunda utambulisho wa Australia tangu makazi ya Uingereza.

Tarehe zilizowekwa

Siku ya Mwaka Mpya 1 Januari

Sisi husherehekea mwanzo wa mwaka mpya.

Siku ya Australia 26 Januari

Sisi husherehekea inamaanisha nini kuwa Mwaustralia na tunakumbuka kuwasili kwa Kundi la Kwanza la Meli (First Fleet) huko Sydney Cove mnamo 1788.

Siku ya Anzac 25 Aprili

Sisi hukumbuka kutua kwa Askari wa Jeshi wa Australia na New Zealand (ANZAC) huko Gallipoli wakati wa Vita vya I vya Dunia. Sisi pia huheshimu Waaustralia ambao wametumikia na kufa katika mizozo.

Sikukuu ya Krismasi 25 Desemba

Siku ya kupeana zawadi kwenye msingi wa sherehe za Kikristo za kuzaliwa kwake Yesu Kristo.

Siku ya Kufungua Zawadi 26 Desemba

Sehemu ya sherehe za Krismasi.

Viwango vinavyobadilika

Siku ya Wafanyikazi au Siku ya Masaa Nane

Husherehekea wafanyikazi wa Australia kushinda siku ya kazi ya masaa nane – kwanza katika ulimwengu.

Pasaka

Hukumbuka hadithi ya Kikristo ya kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Siku ya kuzaliwa ya Malkia

Husherehekea kuzaliwa kwa Mkuu wa Nchi ya Australia, Malkia Elizabeth II. Sherehe hii hufanywa siku ya pili Jumatatu mnamo Juni katika kila jimbo na wilaya isipokuwa Australia Magharibi.

Siku kuu zingine za umma

Siku kuu zingine za umma hufanywa katika majimbo, wilaya na miji. Kwa mfano, Wilaya Kuu ya Australia ina Siku ya Canberra, Australia Kusini ina Siku ya watu wa Kujitolea na Australia Magharibi ina Siku ya Wakfu.

Usiku wa kuamkia Mwaka Mpya fataki juu ya Sydney Harbour 2005

Watu wa Australia

Australia ina idadi ya watu ya karibu milioni 22 na ni mmojawapo ya jamii anuwai ulimwenguni. Watu wa asili wapo asilimia 2.5 ya idadi ya jumla. Zaidi ya robo moja ya wakazi wa Australia walizaliwa ng'ambo, na wamehamia hapa kutoka nchi zaidi ya 200. Utofauti wa idadi ya watu hupeana Australia lugha, imani, mila na tamaduni anuwai.

Miungano rasmi ya Australia na Briteni Kuu imepotea baada ya muda lakini ushawishi wa Briteni Kuu huishi katika taasisi za Australia. Huwa pia inaishi katika thamani zetu nyingi na, hakika, katika lugha yetu ya kitaifa. Wakati zaidi ya lugha 200 zinazungumziwa nyumbani na katika jamii (pamoja na lugha nyingi tofauti za asili), Kiingereza ni sehemu muhimu ya utambulisho wa kitaifa.

Uchumi wa Australia

Australia ina uchumi thabiti na wa ushindani. Tunathamini kazi yetu ya nguvu na yenye ustadi. Ubora wa maisha unaofurahiwa na watu wa Australia ni moja ya hali ya juu ulimwenguni.

Dick Smith (alizaliwa 1944)

Dick Smith ni mwanabiashara anayeongoza Australia, mpenda vituko na mfadhili.

Dick Smith alipata mali yake ya kwanza katika biashara ya elektroniki. Ametumia mali yake kuendeleza Australia. Alianzisha kampuni ya chakula ya Australia kipekee na amewekeza mamilioni ya madola kusaidia kampuni zilizomilikiwa na Australia.

Alitangazwa Mwaustralia wa Mwaka wa 1986 na ameshinda tuzo la maendeleo ya kiufundi na uhifadhi wa mazingira. Alikuwa mtu wa kwanza kuvuka Australia, na Bahari la Tasman, kutumia Baluni ya hewa moto. Anajulikana kwa roho yake ya kupenda vituko, mafanikio yake katika biashara na upendo wake wa ndani wa Australia.

Soko

Taasisi thabiti na za kisasa za Australia na sheria kali za ushuru na biashara hupeana uhakika kwa shughuli za biashara. Tasnia ya huduma, ambayo ni pamoja na utalii, elimu na huduma za kipesa, huunda karibu asilimia 70 ya Australia's Gross Domestic Product (GDP).

Uthabiti wa uchumi wa Australia huifanya iwe mahali pa kupendeza kwa uwekezaji. Soko ya hisa la Australia ndilo la pili kubwa katika eneo la Asia-Pasifiki baada ya Japani.

Biashara

Wabia wakubwa zaidi wa biashara wa Australia ni Japani, Uchina, Amerika, Korea Kusini, New Zealand na Uingereza. Sisi ndio wasafirishaji wakubwa wa ngano, manyoya, mbale ya chuma, madini na dhahabu. Sisi pia husafirisha kawi kwa njia ya gesi ya maji asili na kaa. Uchumi wetu uko wazi na biashara sikuzote imekuwa sehemu muhimu wa ufanisi wa uchumi wetu. Mahuruji ya Australia hivi karibuni yalikuwa jumla ya bilioni $200.

Uchimbaji

Australia ina rasilimali asili nyingi kama kaa, shaba, gesi asili yenye maji na michanga ya madini. Hizi zinahitajika sana, haswa katika kukuza uchumi huko Asia.

Sekta kubwa ya mahuruji ya Australia ni madini na mafuta

Australia kama raia wa ulimwengu

Australia inajivunia jukumu lake kama raia mzuri wa kimataifa. Tunaonyesha hii kwa kusaidia wale wasiojiweza zaidi na sisi ulimwenguni.

Msaada wa kimataifa wa Australia na bidii ya wafadhili.

Mpango wa msaada wa kimataifa wa Serikali ya Australia husaidia nchi zinazoendelea kupunguza umaskini na kufikia maendeleo endelevu. Sisi hutoa msaada huu katika mkoa wetu na ulimwenguni kwa kusaidia watu na serikali.

Waaustralia huonyesha upendo mkubwa wakati janga linatokea katika nchi yetu na ng'ambo. Sisi pia huchanga mara kwa mara kwa nchi zinazopitia shida inayoendelea. Australia kujitolea kwa mpango wetu wa msaada inaonyesha desturi hii ya ukarimu ya Australia.

Oparesheni ya msaada ya Australia huko Indoneshia baada ya sunami ya Bara Hindi mnamo 2004

Kuhusika kiamilifu cha Australia katika mabadiliko ya kimataifa.

Australia imekuwa mwanachama amilifu wa Umoja wa Mataifa (UN) kuanzia mwanzo wake mnamo 1945. Chini ya Kongamano la Wakimbizi wa UN 1951, Australia inatoa ulinzi kwa watu ambao wametambuliwa kama wakimbizi chini ya Kongamano la Wakimbizi wa UN. Sisi pia huchangia juhudi za kuleta amani za UN na wahisani na majibu ya dharura kwa nchi zinazoendelea, na zinahusika sana katika Shirika la Umoja wa Mataifa za Elimu, Sayansi na Utamaduni.

Mnamo 1971, Australia ilikuwa mwanachama kamili wa Shirika la Kichumi na Ukuzani (OECD) Organisation for Economic Cooperation and Development. OCED inalenga kuboresha hali za kichumi, kijamii na ajira katika nchi zake 30 za uanachama na katika nchi zingine zinazoendelea. Wakati huo huo, OECD inalenga kupanua biashara ulimwenguni.

Australia inasaidia sana ushirika wa karibu katika eneo la Asia Pasifiki. Australia ni mwanachama amilifu wa Shirika la Asia Pasifiki (APEC), East Asia Summit (EAS), ASEAN Regional Forum (ARF) na Pacific Islands Forum (PIF).

Dr Catherine Hamlin AC (alizaliwa 1924)

Dr Catherine Hamlin ni daktari wa uzazi, anayejulikana kwa kuokoa wanawake wachanga wa Ethiopia kutokana na maisha ya kusumbuka.

Tangu 1959, Catherine Hamlin amefanya kazi huko Addis Ababa Ethiopia akisaidia wanawake na jeraha la kuzaa linalojulikana kama nasuli ya uzazi 'obstetric fistula' Wanawake wenye tatizo hili hawawezi kuthibiti vile mwili wao unafanya kazi na wanafanywa kutengwa na jamii.

Catherine na mume wake walianzisha Hospitali ya Fistula Addis Ababa. Juhudi zao zimefaa maelfu ya wanawake ambao wanaweza kurudi nyumbani kuishi maisha kamili, yenye afya katika vijiji vyao.

Mnamo 1995, Dr Catherine Hamlin alifanywa Mwenzi wa Mpangilio wa Australia (Companion of the Order of Australia), tuzo kubwa zaidi la Australia. Anaendelea kufanya kazi kwa wanawake Ethiopia.

Australia leo ni nchi kubwa na inayokua, inajivunia mafanikio yake kwenye michezo, sanaa na sayansi. Tunathamini ubora wa maisha ya watu, lakini huwa tunalenga juu kila wakati.

Kupitia msaada wa kimataifa na ukuzaji, Australia imeendeleza hisia yake ya bila mapendeleo kupita uga wa michezo kwenda kwa jamii ya ulimwengu.

Tuzo za Nobel za Australia

Australia inajulikana kwa utafiti wake wa kisayansi na kimatibabu. Waaustralia kumi wametuzwa Tuzo la Nobel katika nyuga hizi.

Professor William Bragg (1862 – 1942) na Lawrence Bragg (1890 – 1971) Mtaalam wa fizikia.

William Bragg (baba) na Lawrence Bragg (mwanawe) walikuwa washindi pamoja wa Tuzo la Nobel katika Fizikia 1915, 'kwa huduma zao katika uchunguzi wa muundo wa fuwele kwa kutumia X-ray'.

Sir Howard Walter Florey (1898 – 1968) Mwanapatholojia.

Alizaliwa huko Adelide, Australia Kusini, Howard Florey alipokea Tuzo la Nobel katika Saikolojia au Matibabu 1945 (pamoja) 'kwa kugundua penisillini na athari zake za kuponya katika magonjwa kadhaa ya kuambukiza'.

Sir Frank Macfarlane Burnet (1899 – 1985) Mwanasayansi wa matibabu na Mwanabaiolojia.

Alizaliwa Victoria, Frank Burnet alituzwa Tuzo la Nobel katika Utaalam wa mwili au Matibabu 1960 (pamoja) 'kwa kugundua uwezo wa kustahimili wa kinga'.

Sir John Carew Eccles (1903 – 1997) Mwanafiziolojia.

John Eccles alizaliwa huko Melborne na alipokea Tuzo la Nobel katika Fiziolojia au Matibabu 1963 (pamoja) 'kwa ugunduzi kuhusu mitambo ya ioni unaohusika katika usisimiaji na kuzuia sehemu za kati na za ukingoni za utando wa seli ya neva'.

Professor John Warcup Cornforth (1917 – 2007) Mkemia.

John Cornforth alizaliwa huko Sydney na alipokea Tuzo la Nobel katika Kemia 1975 (pamoja) 'kwa kazi yake katika stiriokemia athari zinzowezeshwa na kimengenya'.

Professor Peter Doherty (born 1940) Mtaalam wa kinga.

Peter Doherty alizaliwa huko Queensland na alipokea Tuzo la Nobel katika Fiziolojia au Matibabu 1996 (pamoja) 'kwa ugunduzi kuhusu umaalum wa kinga ya seli'.

Professor Barry Marshall (born 1951) Mtaalam wa tiba ya tumbo na Doctor Robin Warren (alizaliwa 1937) Mwanapatholijia.

Professor Barry Marshall na Robin Warren walikuwa washindi pamoja wa Tuzo la Nobel katika Fiziolijia au Matibabu 2005 kwa ugunduzi wao wa 'bacterium Helicobacter' na jukumu lake katika ugonjwa wa majitumbo na kidonda cha tumbo'.

Professor Elizabeth Helen Blackburn (alizaliwa 1948) Mwanabaiolojia.

Professor Elizabeth Helen Blackburn alizaliwa huko Hobart na alipokea Tuzo la Nobel katika Fiziolojia au Matibabu 2009 (pamoja) 'kwa ugunduzi wa jinsi kromosomu hulindwa na telomeres na vimengenyo vya enzyme telomerase'.

Australia pia ina mshindi mmoja wa Tuzo la Nobel katika Fasihi.

Patrick White (1912 – 1990) Mwandishi wa Riwaya na Michezo ya kuigiza.

Alizaliwa London kwa Wazazi wa Australia, Patrick White alituzwa Tuzo la Nobel katika Fasihi mnamo 1973 'kwa sanaa ya kusimulia hadithi ya kubuni na ya kisaikolojia ambayo imetambulisha bara mpya kwa fasihi.



Sehemu ya 5
Historia yetu ya Australia

Tamaduni za asili za Australia ndizo za zamani kabisa zinazoendelea katika ulimwengu.

Historia yetu ya Australia

Historia fupi ya Australia sio hadithi kamili, lakini itakupa wazo la matukio ambayo yameunda nchi yetu na utamaduni wetu. Kwa maelfu ya miaka nchi ilikaliwa na kutunzwa na watu wa asili. Kuwasili kwa Kundi la Kwanza la Meli (First Fleet in 1788) kulimaanisha ulimwengu ungebadilika milele. Muda wote wa miaka 200 iliyopita, Australia imejifunza mambo mengi kuhusu usawa na haki za binadamu kwenye njia ya kuelekea utamaduni anuwai na upatanisho. Mabadiliko ambayo tumefanya yanamaanisha kwamba jamii ya Australia ambayo sasa unaingana nayo ni jamii ambayo mtu huhisi kujumuishwa na kuthaminiwa.

Waaustralia wa asili

Tamaduni za asili za Australia ndizo za zamani kabisa zinazoendelea katika ulimwengu. Watu wa asili wa Australia wameishi hapa kati ya miaka 40 000 na 60 000.

Tamaduni za asili na za visiwa vya Torres Strait zinatofautiana zenyewe. Zina lugha zao na utamaduni wao.

Kihistoria, watu wa asili wanatoka katika nchi kuu ya Australia na Tasmania. Watu wa visiwa vya Torres Strait wanatoka kwenye visiwa kati ya ncha ya Queensland na Papua New Gunea. Watu wa visiwa vya Torres Strait hushiriki tamaduni nyingi sawa na watu wa Papua New Guinea na visiwa vingine vya Pasifiki.

Lugha

Kabla ya makazi ya Briteni, zaidi ya lugha 700 na lahaja zilitumiwa na watu wa asili na wa visiwa vya Torres Strait. Karibu lugha 145 bado zinatumika leo. Hakukuwa na lugha ya kuandikwa. Historia za kuzungumza za utamaduni wa asili ni muhimu sana kwa sababu zinasema hadithi ya watu na nchi. Kwa mfano, hadithi kama zile zinazofafanua kufurika kwa Port Phillip Bay huko Victoria kunamaanisha tukio haswa liliotendeka miaka 10 000 iliyopita.

Kuota ndoto na sanaa za asili

Ukoo tofauti za asili zina jina lao la ile ambayo sisi tuaita kwa Kiingereza ‘Kuota’. Kuota au, Wakati wa kuota, ni mfumo wa maarifa, imani na desturi ambazo zinaongoza maisha ya asili. Inaonyesha watu jinsi wanapaswa kuishi na jinsi wanapaswa kutenda. Watu wasiofuata sheria zake huadhibiwa.

Sanaa za watu wa asili wa Kakadu

Hadithi za Kuota zilielezewa kwa watoto na wazazi wao na wakubwa wao. Hadithi hizi zilifunza watoto jinsi nchi yao iliundwa na kukaliwa, na jinsi ya kutenda na kwa nini. Hadithi pia ziliwapa watoto wao mafunzo ya thamani ya kweli, kwa mfano mahali pa kupata chakula.

Muziki wa asili, wimbo na densi hueleza hadithi ya Kuota na maisha ya kila siku. Wakati watu wa asili huimba na kucheza, wanahisi kuungana na mababu zao.

Aina asili ya sanaa za watu wa asili zilikuwa sanamu au michoro ya mawe na miundo ya ardhi. Baadhi ya hizi ni miaka 30 000. Watu kutoka Australia Kati walichora picha na madoa doa na mviringo kutoa mfano wa nchi au hadithi kutoka kwa Kuota. Wale katika sehemu za kaskazini za Australia walichora picha za watu, wanyama na mapepo.

Kuota huendelea kuwa muhimu kwa watu wa asili leo.

Waulaya wa kwanza kwa Australia

Ugunduzi wa Mapema wa Ulaya

Mnamo karne ya 17, wagunduzi wa Ulaya waligundua sehemu wanazoita 'Terra Australis Incognita', nchi isiyojulikana ya kusini. Mnamo 1606 Mholanzi, Willem Janszoon, alichora ramani sehemu ya magharibi ya Cape York Peninsula huko ncha ya kaskazini Australia. Wakati huu, Luis Vaez de Torres kutoka kwa Urenoi alipitia mlango bahari kaskazini mwa bara.

Baadaye mnamo 1600, wanabaharia wa Uholanzi waligundua pwani ya Magharibi ya Australia. Waholanzi waliita nchi hii' 'Uholanzi Mpya'.

Mnamo 1642, Abel Tasman aligundua pwani ya nchi mpya ambayo aliita 'Van Diemen's Land' (sasa Tasmania). Pia alichora ramani maelfu ya maili ya pwani za Australia. Ramani yake ambayo haijakamilika inaonyesha kwamba aliamini nchi ilikuwa imeunganishwa kwa Papua New Guinea huko kaskazini.

William Dampier alikuwa wa Mwingereza wa kwanza kutembea juu ya ardhi ya Australia. Mnamo 1684, alitua kwenye kaskazini magharibi pwani. Nchi ilikuwa kavu na yenye vumbi kwa hivyo hakuiona muhimu kwa biashara au makazi.

Captain James Cook

Australia pwani mashariki haikugunduliwa na Waulaya hadi Mwingereza James Cook alipoifikia mnamo 1770 katika meli yake, 'Endeavour'. Cook ametumwa na Serikali ya Briteni kwenye safari ya kugundua huko Pasifiki Kusini. Alikodisha pwani mashariki na kutua huko Botany Bay, kusini kutoka Sydney ya kisasa. James Cook aliita nchi hii 'New South Wales', na aliidai kwa King George III.

Ramani ya Abel Tasman wa New Holland, 1644

Usafiri wa wafungwa

Australia ni ya kipekee kwamba wakazi wao wengi wa kwanza wa Ulaya walikuwa wafungwa. Baada ya Amerika walifikia uhuru, Briteni Kuu haingeweza tena kutuma wafungwa huko. Jela za Briteni zilijaa sana. Wakati idadi ya wafungwa iliongezeka, Serikali ya Briteni ilibidi itafute mahali mpya kwao. Mnamo 1786, Briteni Kuu iliamua kutuma wafungwa wake kwa koloni mpya ya New South Wales. Hii iliitwa 'uchukuzi'.

Koloni ya kwanza

Gavana wa kwanza ya koloni ya New South Wales alikuwa Captain Arthur Phillip. Alileta kundi la kwanza la meli 11 salama kutoka Briteni kwa upande mwingine wa ulimwengu. Alichunga kulisha na masilahi ya wafungwa na wachache sana walikufa kwenye safari.

Kapteni Philip aliongoza Kundi la kwanza la Meli (First Fleet) kwenda Sydney Cove mnamo 26 Januari 1788. Ni wakati wa ukumbusho wa siku hii ambayo tunasherehekea Siku ya Australia kila mwaka.

Kundi la Kwanza la Meli (First Fleet) kutoka Briteni, ikiwasili kutoka Sydney Cove mnamo 1788

Miaka ya mapema

Miaka ya mapema ya makazi ilikuwa migumu sana. Gavana Philip alihakikisha kwamba watu hawakukosa chakula kwa kuweka kila mtu kwenye kipimo sawa, pamoja na yeye na maafisa wake. Mawazo ya kawaida na bidii zake zilisaidia koloni kuishi katika miaka hiyo migumu.

Kazi ngumu ya makazi ya mapema ilifanywa na kazi ya lazima ya wafungwa. Walichapwa ikiwa hawakufanya kazi ngumu au ikiwa walikimbia au wangehepa. Ikiwa walifanya uhalifu mkali, walitumwa kwa makazi ya mashambani au kunyongwa. Wafungwa ambao walikamilisha vifungo vyao walikuwa wanaume na wanawake huru na walienda kwa jamii ya kufanya kazi na kukuza familia.

Fursa Mpya

Idadi ya kwanza ya Ulaya wa Australia ni Waingereza, Waskoti, watu wa Welshi na Wairishi. Waskoti, Welshi na Wairishi wamekuwa vitani na Waingereza hapo zamani, lakini huko Australia vikundi vinee viliishi na kufanya kazi karibu pamoja.

Wafungwa na wafungwa wa zamani walianza kupata fursa mpya kwenye koloni. Maafisa wa jeshi walitumia wakati wao kutengeneza pesa kwa kuuza na kutuma wafungwa na wafungwa wa zamani kuwasaidia. Hivi karibuni, baadhi ya wafungwa wa zamani waliweka biashara zao wenyewe kuwa wafanyi biashara. Wafungwa wa zamani wengine walifanya vyema kama wakulima, wanabiashara, wauzaji duka nawenye baa. Wanawake wafungwa wa zamani walifanya vyema katika biashara na katika njia nyingi walifurahia uhuru zaidi kuliko huko Uingereza.

Caroline Chisholm (1808 – 1877)

Caroline Chisholm alikuwa kiongozi mbadilishaji wa kijamii ambaye huboresha hali hiyo ya wanawake wa siku za mapema za koloni.

Caroline alikuja Australia na mume wake afisa wa jeshi na watoto watano mnamo 1838. Alisaidia wanawake wahamiaji ambao waliishi kwenye mitaa ya Sydney. Katika miaka michache, aliunda hosteli 16 za wanawake wahamiaji karibu na koloni.

Caroline alifanya bidii kuboresha maisha kwenye meli kwa watu wanaosafiri kwenda kwa koloni. Alipanga pia mpango wa mkopo kwa watu wasio na mali kuwasaidia kuvunja mzunguko wa kutegemea na umaskini.

Leo, shule nyingi za Australia ziliitwa majina ya Caroline Chisholm. Alijulikana kama 'rafiki wa wahamiaji' na anakumbukwa kwa juhudi zao kusaidia watu kuanza maisha mapya.

Gavana aliyeelimishwa

Pamoja na Gavana Philip, Governor Lachlan Macquarie ana cheo muhimu katika historia yetu ya mapema. Aliongoza koloni ya New South Wales kati ya 1810 na 1821. Alikuza koloni kama makazi huru, sio koloni ya wafungwa. Aliboresha shughuli za ukulima na kujenga barabara mpya na vifaa vya umma. Alihimiza uvumbuzi wa Australia.

Macquarie pia aliweka pesa kwa elimu na aliheshimu haki za wafungwa. Aliwapa wafungwa wa zamani kazi kama majaji na watumishi wa umma.

Gavana Macquarie anaheshimiwa katika historia kwa mabadiliko mazuri aliyofanya kwa koloni. Chuo kikuu cha Macquarie huko New South Wales kimepewa jina lake.

Urithi wetu wa wafungwa

Baada ya muda wa Macquarie, ilifikiriwa kwamba cheo cha Gavana kilikuwa cha nguvu sana kwa mtu mmoja, kwa hivyo manmo 1823, Baraza la Watunga Sheria wa New South Wales ilianzishwa kushauri Gavana anayefuata. Baraza la Watunga Sheria basi walijaribu kubadili koloni ili wafungwa waliadhibiwa vyema na hawakuishi vizuri sana. Walakini haingeweza kufungia fursa zote kwa wafungwa wanaoishi huko New South Wales na koloni zingine zilizoanzishwa karibu na Australia katika karne ya 19.

Kwa pamoja, zaidi ya wafungwa 160 000 walisafirishwa kwenda Australia. Briteni kuu iliacha kutuma wafungwa kwenda New South Wales mnamo 1840, kwenda Tasmania mnamo 1852 na kwenda Australia Magharibi mnamo 1868.

Watoto wa wafungwa wamekuwa huru kila wakati, kwa hivyo utengano kati ya wafungwa wa zamani na wakazi ulipungua pole pole. Kuanzia 1850, wakoloni walijiongoza na walitaka kujenga jamii za kuheshimika. Wakoloni waliaibika kwa sababu ya mababu wao wa kufungwa na hawakuongea kuzihusu. Karibu karne moja baadaye, hisia hii ya kuaibika ilibadilika. Waaustralia walianza kujivunia mwanzo wao wa kuwa wafungwa na watu wengi wao sasa wanafurahia kugundua wana mababu wafungwa.

Katika moyo wa kukubali, Waaustralia wamekuwa watu ambao hawajali sana juu ya asili ya familia ya mtu au tabia ya zamani. Sisi hupeleka watu kukutana nao na kuwapa watu 'kutendewa sawa'.

Watu wa asili baada ya makazi ya Waulaya

Inakadiriwa kwamba kulikuwa kati ya 750 000 na milioni 1.4 watu wa asili na wa visiwa vya Torres Strait huko Australia mwanzo wa makazi ya Ulaya. Idadi inaweza kujumuishwa karibu nchi 250 binafsi na zaidi ya vikundi 700 vya lugha.

Wakati walikaa kwanza huko Australia, Serikali ya Briteni haikufanya muungano na watu wa asili. Watu wa asili walikuwa na uchumi wao na muungano wa zamani nchini. Serikali haingeweza kugundua hii kwa sababu hakukuwa na mifumo kama hiyo au imani kama hizo Ulaya. Watu wa asili hawakulima mimea au kupanga nyumba zao katika sehemu moja kama vile Waingereza walivyofanya, kwa hivyo Serikali ilifikiri hawakukuwa na hisia ya umiliki. Serikali ilihisi huru kutawala nchi.

Athari mbaya ya kufa

Magavana wa mapema waliambiwa wasiwadhuru watu wa asili, lakini wakazi wa Uingereza walienda kwa nchi ya watu wa asili na wengi wao waliuawa. Wakazi kawaida hawakuadhibiwa kwa kutenda uhalifu huo.

Baadhi ya watu wa asili na wakazi wa Ulaya waliweza kuishi kwa amani pamoja. Baadhi ya wakazi waliajiri watu wa asili kwenye mashamba ya kondoo na ngombe. Gavana Macquarie alipea watu wa asili nchi yao wenyewe kwa ukulima na kuanzisha shule ya watoto wa asili. Walakini, ni watu wachache mno wa asili huishi njia ambavyo wakazi waliishi. Hawakutaka kupoteza mila zao za kitamaduni.

Hatujui ni watu wangapi wa asili waliuawa katika vita juu ya ardhi lakini tunajua kwamba mamia ya maelfu ya watu wa asili waliuawa. Wauwaji wakubwa wa watu wa asili walikuwa magonjwa ambayo Waulaya walileta nchini. Kupoteza maisha ya watu wa asili ilikuwa mbaya sana. Huko Victoria mnamo 1830, idadi ya watu wa asili ilikuwa karibu watu 10 000. Mnamo 1853, watu 1907 wa asilia tu walihesabiwa.

Hatua za kihistoria

Ugunduzi wa kindani

Huko New South Wales, wakoloni wapya walikumbana na ugumu mkubwa. Ni sehemu ndogo sana ya Australia ambayo ni nchi yenye rotuba. Watu wa asili walijifunza kujisimamia na kuishi katika mazingira haya, ingawa waliumia pia katika nyakati za ukame.

Kizuizi cha kwanza cha wakazi wa Sydney walikutana nacho katika kugundua nchi ya ndani ilikuwa safu ya mlima kilomita 50 magharibi mwa Sydney, Blue Mountains. Mnamo 1813, wanaume watatu, Blaxland, Wentworth na Lawson, mwishowe walivuka milima. Barabara na reli kote kwenye Blue Mountains bado hufuata njia waliouchukua.

Kwenye upande mwingine wa milima hii wagunduzi waligundua nchi wazi ambayo ilikuwa nzuri kwa kufuga kondoo na ngombe. Ndani ya nchi, walakini, walikutana na nchi yenye nyika kavu. Walitatizika kupata maji na kubeba chakula cha kutosha kuishi. Mgunduzi mzaliwa wa Ujerumani, Ludwig Leichhardt, alipotea alipokuwa anajaribu kuvuka bara kutoka mashariki kwenda magharibi mnamo 1848.

Mnamo 1860 Burke na Wills waliondoka kwa Melbourne kupitia Australia kutoka kusini kwenda kaskazini. Waliongoza uchunguzi mkubwa lakini njia za kuvuka likuwa ngumu sana. Burke na Wills hawakuwa wana wenye uzoefu wa pori. Walipokea msaada kutoka kwa watu wa asili wa Yandruwandha lakini wagunduzi wote wawili waliaga duniani walipokuwa wanarudi. Hata ingawa Burke na Wills walikosa kukamilisha ugunduzi wao, hadithi yao hukumbukwa katika sanaa na fasihi. Ni mfano tanzia wa ugumu wa nchi yetu.

Ugunduzi wa Burke na Wills kuvuka Australia, 1860

Wakazi na waanzilishi

Hata wakati wakazi walikuwa na nchi nzuri, maisha yalikuwa magumu sana. Baada ya muda wa mafuriko na ukame, wakulima mara nyingi walihitaji kuanza tena. Kufikia 1838, manyoya yalikuwa mahuruji kuu ya Australia na ikiwa kulikuwa na ukame au ikiwa bei ya ng'ambo ya manyoya ilianguka, wakazi wangepoteza mapato yao. Walakini, watu walijibeba na kuendelea kupigana. 'Mipiganaji wa Aussie' ndilo jina lililopewa mtu ambaye aliponea nyakati ngumu. Mpiganaji wa Aussie analeta mfano wa moyo wa kupigana na kuvumilia wa Australia. Waanzilishi wanawake na wanaume wanaheshimiwa kwa ujasiri wao wakati wa nyakati ngumu hizo. Mara nyingi wanawake huweka biashara zao au shamba zao wakati wanaume wameenda mbali au wameaga duniani.

Ilikuwa wakati wa miaka mibaya hii ya mapema ambayo moyo wa Australia wa kujali ulianza. Ilikuwa ya nguvu kati ya wanaume waliosafiri kupitia porini, kunyoa na kuchunga kondoo. Wakazi pia walisaidiana kwa sababu ya ugumu. Mila hii bado ni sehemu ya maisha ya Australia, kwa mfano maelfu ya watu wamejitolea kupigana na moto ya msitu kila mwaka.

Mbio ya dhahabu

Ugunduzi wa dhahabu huko NSW mapema 1851 umefafanuliwa kama 'ugunduzi uliobadilisha taifa'. Muda mfupi baadaye, dhahabu ilipatikana huko Victoria, koloni mpya ya kujitegemea.

Mwisho wa 1852, watu 90 000 walikuwa wamesafiri kwenda Victoria kutoka sehemu zote za Australia na kote ulimwenguni kutafuta dhahabu.

Dhahabu iligunduliwa kwanza katika koloni za New South Wales na Victoria mnamo 1851

Vita vya Eureka vinakumbukwa kama wakati mkubwa wa kidemokrasia katika historia ya Australia. Katika machimbo wa dhahabu wa Ballarat mnamo 1854, wachimbaji dhahabu walifanya maandamano dhidi ya njia mbaya ambayo maafisa wa serikali waliendesha machimbo wa dhahabu.

Majeshi ya serikali wangekuwa wakali na wachimbaji wakati walikusanya ada ya leseni ya kuchimba dhahabu. Mnamo 11 Novemba 1854, watu 10 000 walikusanya katika Bakery Hill, Ballarat, kubadili hati kwa haki muhimu za kidemokrasia. Walitaka kuweza kuchimba dhahabu bila kuhitaji kulipia leseni ghali. Walitaka pia kupiga kura kwa watu kuwawakilisha katika Bunge la Victoria.

Kundi ndogo lilijenga boma huko machimbo za Eureka na walipeperusha bendera yao ya kupinga na Msalaba wa Kusini juu yake. Maafisa wa serikali walituma askari kuvamia hifadhi asubuhi ya 3 Desemba 1854. Wachimbaji wa dhahabu walishindwa na karibu watu 30 waliuawa.



Bendera ya Eureka

Wakati viongozi wa upinzani waliwekwa kwenye jaribio kwa uhaini mkubwa, hakuna baraza la wazee wa mahakama lingewahukumu. Tume ya Kifalme iliamua serikali kuwa na makosa na mahitaji mengi ya wachimbaji yalitimizwa. Ombi lao la kuwakilishwa kisiasa lilitimizwa pia. Kati ya mwaka mmoja, Peter Lalor, kiongozi wa wapinzani, alikuwa mwanachama wa Bunge la Victoria.

Kwa miaka mingi, upinzani wa Eureka umekuwa ishara ya upinzani na imani yetu katika kutopendelea.

Mbio ya dhahabu ilibadilisha Australia katika njia nyingi. Wakati wa miaka ya mbio ya dhahabu, idadi ya watu wa Australia iliongezeka kuanzia 43 000 mnamo 1851 hadi milioni 1.7 mnamo 1870. Reli na telegrafu ya kwanza ziliundwa mnamo 1850 kuunganisha idadi iliyokua.

Mabaki makubwa ya dhahabu yalipatikana katika koloni zote isipokuwa Australia Kusini. Uchumi ulinawiri na dhahabu ilipita manyoya kama mahuruji yetu ya thamani zaidi. Kufikia 1890, inawezekana kwamba Australia ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kuishi ulimwenguni.

Maskwota na wakulima

Kuanzia siku za mapema za wakoloni, watu wanaojulikana kama 'maskwota' walikuwa wamechukua eneo kubwa la nchi kulima. Ingawa hawakulipia shamba hili, maskwota waliichukulia kama yao. Baada ya mbio za kwanza za dhahabu kuisha, kulikuwa na mvutano mkubwa wa kuchukua shamba kutoka kwa maskwota.

Mnamo 1860, Serikali ilitaka kuuzia shamba la maskwota kwa wanaume wanaofanya kazi na familia zao kulima. Maskwota walijaribu kujiwekea shamba kubwa wawezavyo kwa kudai kupangisha kwingi, haswa zile ambazo zilikuwa kwenye sehemu bora.

Wakulima wapya walikumbwa na mazingira magumu na hadi reli zilipojengwa, walikuwa mbali na soko. Fursa ya kupata mapato ya juu jijini kawaida ilifanya maisha kwenye shambani na kufanya kazi kutoa mapato kidogo, yasiyopendeza.

Walakini, wakulima walifanya vyema Australia Kusini, na mila ya Australia ya kuvumbua mashine kufanya ukulima uwe rahisi ulianza hapo. Kwa mfano, jembe la stump-jump (1870), liliruhusu ardhi mbaya kufyekwa kwa ukulima wa mimea.

Uhamaji mnamo 1800

Mapema 1800, wakazi wa Waingereza, Waskoti, Welshi na Wairishi walikuwa makundi makuu katika koloni. Urithi wao ulikuwa kwa msingi wa taifa mpya. Burudani, shughuli za kitamaduni na kidini za Australia zilikuwa sawa na za Uingereza. Walakini, kulikuwa pia na vikundi vidogo vya wahamiaji kutoka Ulaya na Asia. Waulaya waliowasili mnamo 1800 ni pamoja na Waitaliano, Wagiriki, Wapole, Maltese na Warusi na vile vile wakazi wa Ufaransa katika tasnia ya mvinyo. Hizi zilikuwa haswa wanaume vijana wanaotafuta kazi na mali, au wabaharia ambao waliacha meli zao.

Wahamiaji wa Uchina walianza kuwasili Australia baada ya 1842. Idadi yao iliongezeka baada ya ugunduzi wa dhahabu na kulikuwa na mvutano wa rangi kwenye machimbo ya dhahabu. Hiipengine ilisababisha vurugu dhidi ya Wachina, kama vile wale Bendigo mnamo 1854. Mivutano ya rangi ilisababisha vizuizi kwenye uhamaji wa Victoria mnamo 1855 na New South Wales mnamo 1861.

Baada ya mbio za dhahabu za 1850, Wachina wengi walirudi nyumbani. Kati ya wale waliokaa mahali ni wachina wakulima wa soko ambao walisambaza matunda na mboga katika maeneo ambayo maji yalikuwa nadra.

Kuanzia 1860, watu kutoka Irani, Misri na Turuki walikuja kuendesha 'treni' za ngamia kupitia porini ya Australia. Pamoja na watunza ngamia wa India, walijulikana kama 'Afghans' kwa sababu ya nguo sawa na imani za dini zinazofanana za Kiisilamu. Watunza ngamia hawa walijulikana kama 'waanzilishi wa bara'. Karibu Wahindi 4000 na Watu wa visiwa vya Pasifiki 6000 pia walifanya kazi katika tasnia za sukari na za ndizi huko Queensland.

Kuanzia 1880, wafanyikazi kutoka Lebanon waliwasili Australia. Walebanisi wengi walihusika katika tasnia za vitambaa na nguo. Familia za Lebanisi zilikuja kumiliki biashara nyingi za kuuza nguo katika nchi ya Australia, utamaduni ambao unaendelea hivi leo.

Watunza ngamia wa 'Afghan' katika porini ya Australia

Hifadhi za Watu wa asili

Baada ya vita mapema kati ya watu wa asili na wakazi wa nchi kuisha, watu wa asili waliishi kwenye ukingo wa jamii. Wengine walifanya kazi kwenye vituo vya kondoo na ng'ombe porini kwa mapato madogo sana. Serikali ya ukoloni iliunda hifadhi ambapo watu wa asili wangeweza kuishi, lakini maeneo haya hayakuruhusu watu wa asili kuishi maisha ya kitamaduni. Hawangeweza kuwinda na kukusanya walichotaka.

Mnamo mwisho wa 1800, serikali za ukoloni ziliondoa haki za watu wa asili. Ziliambia watu wa asili mahali pa kuishi. Waliwaambia ni nani wangeweza kuoa na kuolewa na walichukua watoto wengi wa asili kutoka kwa wazazi wao. Watoto hawa walitumwa kwa familia za wazungu au nyumba za serikali za watoto yatima. Desturi hii haiko tena lakini inabaki kuwa sababu ya dhiki kuu kwa watu wa asili na Waaustralia wengi.

Haki ya kupiga kura

'Watetesi wa haki ya kupiga kura' ilikuwa neno lililotumiwa kote ulimwenguni kwa wanawake waliofanya kampeni kwa haki ya kupiga kura katika uchaguzi. Wakati wa 1880 na 1890, kila koloni lilikuwa na angalau jamii moja ya wapigaji kura. Watetesi wa haki ya piga kura walikusanya maelfu ya sahihi kwenye malalamiko kuwakilisha kwa bunge zao za ukoloni.

Wanawake huko Australia Kusini walishinda haki ya kupiga kura na kuomba uchaguzi wa bunge mnamo 1895. Wanawake wa Australia Magharibi walishinda haki ya kupiga kira mnamo 1899.

Mnano 1902, Australia ilikuwa nchi ya kwanza kuwapa wanawake haki ya kupiga kura na haki ya kuchaguliwa kwa Bunge la Australia. Wanawake wa asili (na wanaume) hawakupewa haki ya kupiga kura hadi 1962.

Edith Cowan alikuwa mbunge mwanamke wa kwanza wakati alichaguliwa kwa Bunge la Australia Magharibi mnamo 1923. Ni hadi 1943 ndipo mwanamke, Enid Lyons, aliteuliwa katika Bunge la Australia.

Shirikisho

Koloni zilikuwa zimeanzishwa kando, lakini kufikia karibu mwisho wa karne ya 19 mawazo ya kawaida ya umiliki wa kitaifa yalikuwa yameanza. Hisia hii ilionyeshwa kwa maneno ya 'Endeleza Australia bila Mapendeleo' (Advance Australia Fair). Wimbo huu uliandikwa na Peter Dodds McCormick na kuimbwa kwanza huko Sydney, mnamo 1878. Sasa ni wimbo wetu wa taifa.

Kuelekea mwisho wa karne ya 19, majaribio mawili yalifanywa kuleta koloni karibu. Mnamo 1889, Sir Henry Parkes aliitisha taifa mpya la nguvu kuundwa. Kongamano la Shirikisho la Australia lilifanywa mnamo 1890 kujadili wazo la shirikisho la Australia.

Baada ya kuchelewa, hatua ya shirikisho ilipata kasi mnamo 1893. Wapiga kura walichagua wanachama wa kongamano lililofuata la katiba. Wapiga kura walipiga kura kwa awamu mbili za kura ya maoni na walikubali katiba. Ukweli kwamba mchakato wa shirikisho ulikuwa kwa msingi wa matamanio ya watu ulionyesha jinsi Australia inayoendelea ilikuwa.

Catherine Spence (1825 – 1910)

Catherine Spence alikuwa mwandishi, muhubiri, mtetezi wa wanawake na wa haki za kupiga kura.

Catherine Spence alihamia Australia kutoka Scotland. Aliandika riwaya zilizoshinda tuzo juu ya maisha ya Australia na vitabu vya shule vile vile.

Alisaidia kuunda shirika kusaidia watoto wasiokuwa na makao na kusaidia shule mpya za watoto wadogo na shule za upili za serikali za wasichana.

Alikuwa mwanamke wa kwanza kugombea bungeni na kupokea kura nyingi, lakini hakushinda kiti chake. Mnamo 1891 alikuwa makamu wa Rais wa Ligi ya Wanawake wa Haki ya Kupia Kura ya Australia Kusini (Women's Suffrage League of South Australia).

Catherine Spence ni ishara ya kile wanawake wanaweza kufikia, hata katika nyakati zenye vizuizi.

Siku ya Shirikisho huko Brisbane, 1901

Serikali ya Briteni ilikubali kwamba Australia ingejiongoza yenyewe na Serikali ya kwanza ya Australia iliapishwa mbele ya umati mkubwa huko Uwanja wa Centennial huko Sydney mnamo 1 Januari 1901. Waziri Mkuu wa taifa mpya alikuwa Edmund Barton, ambaye aliongoza hatua ya shirikisho katika New South Wales.

Australia sasa ilikuwa taifa lakini bado ndani ya Ufalme wa Briteni. Haikupata nguvu kamili dhidi ya ulinzi na maswala ya kigeni hadi 1931. Ingawa hisia ya kitaifa ilikuwa imekua, wazo la kuwa Mbriteni bado ilikuwa na nguvu.

Sir Edmund Barton

Kuzaliwa kwa vyama vya kisiasa

Kufikia 1880, wafanyikazi huko Australia walikuwa wamejenga vyama vya nguvu vya wafanyikazi. Katika nyakati ngumu za unyogovu wa uchumi na ukame, vyama hivi viligoma kulinda mapato na hali zao. Kisha wafanyikazi walirudia siasa. Mnamo 1891, waliunda Chama cha Wafanyikazi.

Kazi ya kwanza ya Chama cha Wafanyikazi ilikuwa kurudisha na kuboresha mapato na hali za wafanyikazi. Watu wa kiwango cha katikati waliishi vyema kuliko wafanyikazi lakini walielewa hali ya wafanyikazi. Halmashauri rasmi ziliundwa kuweka mapato na kuzuia migomo. Mnamo 1907, Korti ya Jumuiya ya Madola ya Upatanisho na Maamuzi (Commonwealth Court of Conciliation and Arbitration) iliamua mapato ya chini kadri kwenye kiwango ili mwanamume anayefanya kazi, mke wake na watoto wake watatu waweze kuishi katika faraja 'kiasi'.

Chama cha Wafanyikazi kilipokuwa, vyama vingine vyote viliungana kuwa Chama cha Uhuru mnamo 1910. Chama hiki kimekuwa na majina mengi. Kati ya vita, ilikuwa Chama cha Kitaifa (Nationalist Party) na ndipo Chama cha Umoja Australia (United Australia Party). Mnamo 1944 Chama cha Uhuru tunachojua leo kilianzishwa. Hii ilifuatia kongamano lililofanywa na Robert Menzies ambalo lilihusisha vyama vingi visivyo vya Wafanyikazi. Sir Robert Menzies aliendelea kuwa Waziri Mkuu aliyetumikia sana wa Australia.

Baada ya Vita vya Dunia I, Chama cha Nchi kiliundwa kuendeleza hatua ya wakulima. Inayojulikana sasa kama Wataifa, kawaida hutenda katika muungano na Chama cha Uhuru.

Sheria ya Vizuizi vya Uhamaji 1901

Sera ya 'Mwaustralia Mweupe' ilikuwa sheria wakati *Sheria ya Vizuizi vya Uhamaji 1901* ilipitishwa mnamo Desemba 1901, Hii ilizuia wahamiaji kufanya kazi huko Australia na ilizuia uhamaji wa watu ambao 'hawakuwa weupe'.

Mtu yeyote na asili isiyo ya Ulaya alilazimika kufanya mtihani wa kusoma kwa nguvu maneno 50 kwa lugha ya Ulaya. Wanachama wa Jumba la Kibiashara la Uchina (Chinese Chamber of Commerce), wakili William Ah Ket na wanabiashara Wachina wanaoongoza walipingawazi, lakini haikufaulu katika kubadili sheria.

Wachina, Wahindi, Watu wa visiwa vya Pasifiki na watu kutoka Mashariki Kati walibadilishwa na wahamiaji kutoka Ulayakusini katika Australia mpya iliyoshirikishwa, lakini michango ya kitamaduni ilikuwa sehemu ya utambulisho wa kijamii cha Australia.

Vita vya Dunia I, 1914 – 1918

Kando na vita vidogo kati ya wakazi na watu wa asili, Australia imekuwa nchi yenye imani. Hakujakuwa na vita vya ndani au mapinduzi. Wakazi wa kwanza walikuwa waaminifu sana kwa Ufalme wa Briteni.

Walakini, kama makazi ya mbali ya Ulaya karibu na Asia, Australia pia ilihisi kudhuriwa, haswa baada ya Japani kuwa nguvu kubwa. Australia ilitegemea kwenye Ufalme wa Briteni na nguvu yao ya neva kutukinga. Australia ilipigana katika Vita vya Dunia viwili kufanya Ufalme wa Briteni kuwa wa nguvu na kujilinda sisi wenyewe.

Askari wa Australia iliingia Vita Vya Dunia I mnamo 1915 na uvamizi wa msaidizi wa Ujerumani, Uturuki. Waaustralia na Wanyuzilandiwalipewa sehemu yao kuvamia Gallipoli Peninsula.

Waliwekwa kando na katika sehemu mbaya na walilazimika kupanda milima walipokuwa wanapigwa risasi na majeshi ya Uturuki. Kwa njia fulani, walifika juu ya milima na wakachimba, walakini wanaume wengi walikufa. Waaustralia nyumbani walijivunia katika moyo wa Anzac.

Tarehe ya kutua kwa Gallipoli (25 Aprili) ni siku kuu ya kitaifa. Inaitwa Siku ya Anzac kwa Askari wa Jeshi wa Australia na Nyuzilandi.

Baada ya Gallipoli, jeshi la Australia lilipigana kwenye Mbele ya Magharibi huko Ufaransa. Hapo ndipo walipata jina la 'wachimbaji' kwa sababu walitumia muda mwingi kuchimba na kutengeneza mitaro. Wakiongozwa na kamanda, General John Monash, wachimbaji wa Australia walishinda vita vingi katika vita vya mwisho dhihi ya Ujerumani.

Wanajeshi wa Australia pia walihudumu huko Mashariki ya Kati, walihusika katika ulinzi wa Suez Canal na ushindi wa Uhusiano wa Sinai Peninsula.

Gallipoli Peninsula wakati wa Vita vya Dunia I

Simpson na punda wake – John Simpson Kirkpatrick (1892 – 1915)

John Simpson Kirkpatrick alikuwa mwanajeshi na shujaa wa Australia.

Kama Private John Simpson, alihudumu katika Gallipoli katika askari wa gari za dharura za matibabu kama wabebaji machela. Ilikuwa ngumu kubeba machela kwa milima na mabonde. Kinyume na maagizo ya jeshi, alitumia punda, iliyoitwa Duffy, kusaidia kusafirisha wanajeshi waliojeruhiwa salama.

Usiku na mchana, saa baada ya saa, wangehatarisha maisha yao kwa kusafiri kati ya mapigano na kambi za ufuo.

Private John Simpson alikuwa amewasili Gallipoli mnamo 25 Aprili 1915. Aliuawa wiki nne tu baadaye na bunduki za adui. Wanajeshi kwenye kambi ya ufuo walitazama Duffy kwa huzuni. Bado akibeba wanajeshi waliojeruhiwa, akija kwa ufuo bila mkubwa wake.

Shujaa wa Anzac

Mila ya Anzac iliundwa mnamo 25 Aprili 1915 wakati Askari wa Jeshi wa Australia na Nyuzilandi (ANZAC) walitua Gallipoli Peninsula huko Uturuki.

Ilianzisha mwanzo wa kampeni ambayo ilikaa miezi nane na ilisababisha wahasiriwa 25 000 wa Australia, pamoja na 8700 ambao waliuliwa au kuuawa na majeraha au magonjwa. Ujasiri na roho ya wale waliotumikia Gallipoli Peninsula waliunda ushujaa, na 'Anzac' ilikuwa sehemu ya lugha ya Australia na Nyuzilandi.

Mnamo 1916, ukumbusho wa kwanza wa kutua ulifanywa huko Australia, Nyuzilandi na Uingereza, na majeshi ya Misri vile vile. Katika mwaka huo, 25 Aprili iliitwa 'Siku ya Anzac'.

Kufikia 1920, sherehe za Siku ya Anzac zilifanywa kota Australia na majimbo yalikuwa yametenga Siku ya Anzac kama sikukuu ya umma. Makumbusho kuu ya vita yalijengwa katika miji mikuu, na sanamu katika miji na vijiji kwa taifa lote kukumbuka wanaume na wanawake walioouliwa katika mizozo hiyo na ya baadaye.

Siku ya Anzac sasa ni siku ya kuheshimu wote ambao walihudumu katika vita, mizozo na oparesheni za amani. Sio sherehe ya kijeshi. Haiheshimu ushindi – kampeni ya Gallipoli haikufaulu. Inaheshimu ubora wa wanajeshi: kujali, kuvumilia na ucheshi katika hali ya dhiki. Leo, Siku ya Anzac ilikumbukwa huko Australia na kote ulimwenguni. Wanajeshi wa Australia waliorudi kutoka kwa Vita vya Dunia II na mizozo mingine, na waweka amani na askari wastaafu kutoka kwa nchi zenye Uhusiano, wote huandamana katika gwaride za Siku ya Anzac.

Ibada ya mapambazuko ya Huduma ya Anzac (Anzac Day Dawn Service) huko Gallipoli

Unyogovu Mkubwa, 1929 – 1932

Unyogovu Mkubwa ulikuwa wakati wa ugumu sana kwa watu wa Australia. Ulianza wakati sawa na kuanguka kwa Soko la Hisa la New York (New York Stock Exchange), lakini kulikuwa na mambo mengine pia yaliyosababisha Unyogovu. Hii ni pamoja na kuanguka kwa bei na mauzo ya mahuruji, kuanguka kwa mikopo ya ng'ambo na serikali kutumia na kuanguka kwa ujenzi. Kufikia 1932 katikati, karibu asilimia 32 ya Waaustralia hawakuwa na kazi.

Athari ya Unyogovu kwa jamii ya Australia ulikuwa wa kufadhaisha. Bila kazi na mapato thabiti, watu wengi walipoteza nyumba zao. Walilazimika kuishi katika nyumba duni bila joto au vyoo. Baadhi ya akina baba walitoroka familia zao au walianza kunywa pombe. Watoto wa kiwango cha wafanyakazi walianza kuacha shule katika umri wa miaka 13 hadi 14. Wanawake wengi walifanya kazi za msingi na kulea watoto vile vile na nyumba zao wenyewe.

Wakati huo hiyo kabla Unyogovu, Serikali ya Australia haikuwa na mpango kuu wa ukosefu wa ajira. Kando na ufadhili na baadhi ya mashirika ya binafsi, watu maskini walilazimika kutegemea miradi ya ukosefu wa ajira na kazi za umma.

Uchumi ulianza kuwa bora mnamo 1932, lakini katika hali nyingi, uharibifu kwa familia haungeweza kutengenezwa. Wakati wa Unyogovu Mkubwa, jukumu muhimu la ufadhili wa Australia na wafanyikazi wakujitolea ulihimizwa.

Jikoni la supu wakati wa Unyogovu Mkubwa

Sir Charles Kingsford Smith (1897 - 1935)

Sir Charles Kingsford Smith alikuwa rubani wa kuchukua hatari, mwanzilishi wa masomo ya ufundi wa ndege na shujaa wa Australia.

Katika Vita vya Dunia I, Charles Kingsford Smith alipigana huko Gallipoli na aliendesha ndege na Askari wa Ndege wa Briteni ya Kifalme (Britain's Royal Flying Corps).

Kufanikiwa kwake kubwa kulikuwa kuvuka kwanza kwenda kwa Bahari la Pasifiki kutoka California kwenda Queensland mnamo 1928. Wakati ndege yake, ya Southern Cross, mwishowe iliwasili huko Australia,watu 25 000 wanaopenda walikuwa hapo kushangilia shujaa wao 'Smithy'. Alitolewa kwenye huduma yake ya ndege mnamo 1932.

Kwa bahati mbaya, mnamo 1935, alianguka na ndege yake akiruka kutoka Uingereza kwenda Australia na hakuwahi kupatikana.

Sir Charles Kingsford Smith ameitwa mwanandege maarufu zaidi na anakumbukwa kwa kuwapa watu shujaa wa Australia wa kutazama, kati ya Unyogovu.

Vita vya Kidunia II, 1939 – 1945

Katika Vita vywa Dunia II, Waaustralia walipigana kwa Wahusika kwenye jangwa za Afrika Kaskazini na maeneo mengine. Huko Afrika Kaskazini, walipigana katika vita vya muda mrefu na Wajerumani na Waitaliano katika mji wa Tobruk. Adui aliwaita 'Rats of Tobruk' ('Panya wa Tobruk') kwa sababu walikuwa na hali ngumu na walilazimika kula chakula chochote wangeweza kupata. Waaustralia walipigana na kuponea hali hizi ngumu na kwa hivyo walibadili jina hili wenyewe. Vita hivi vilionyesha kwamba wanaume hawa walikuwa na moyo wa kupigana kama wachimbaji kwa Vita vya Dunia I. Askari wenyewe walijua kwamba walikuwa na desturi ya kuishia.

Baada ya Japani kuvumbua vita katika Pasifiki, wanajeshi wa Australia walikuja nyumbani. Kabla yao kurudi, Papua na New Guinea walihitaji kulindwa. Kazi hii ngumu ilipeanwa kwa wanajeshi wa kawaida na wanajeshi vijana mujibu wa sheria ambao hawakuwa wamefunzwa vyema. Walipigana na adui katika msitu, kwa njia ya wima ya matope inaojulikana kama Kokoda Track. Wanajeshi wa Australia walikomesha uvamizi wa Wajapani na Kokoda Track waliunga Anzac Cove huko Gallipoli kama sehemu ya safari yake kwa Waaustralia wengi.

Askari aliyeumia kwenye Kokoda Track walisaidia na mbeba Papua

Wakati Wajapani walichukua kituo kuu cha jeshi cha Briteni huko Singapore mnamo 1942, wanajeshi 15 000 wa Australia walikuwa kati ya wale ambao walishikwa na kupelekwa kenye Reli ya Thai-Burma. Ilikuwa wakati wa ujenzi wa Reli ya Thai-Burma chini ya Wajapani wakati wa Viya vya Dunia II ambazo maelfu ya wafungwa wa vita wa Australia na Briteni walikufa.

Moja ya makumbusho makali ya vita vya Australia ni kutendewa kubaya kwa wanaume hawa na Wajapani. Ingawa wafungwa wa vita wa Australia walijitahidi kulindana, maafisa na watu wakitendeana kwa usawa, Waaustralia wengi walikufa pia.

Siku ya Ukumbusho

Sherehe za Siku ya Anzac vile vile, Siku ya Ukumbusho pia ni siku ambayo Waaustralia hukumbuka wale ambao walihudumu na kufa kwenye vita. Saa 5 asubuhi (11am) mnamo 11 Novemba (mwezi wa 11) kila mwaka, Waaustralia walisitisha kujitolea kwa wanaume na wanawake ambao walikufa au kuumia katika vita na mizozo, na pia wote waliohudumu vile vile. Sisi huvaa mpopi nyekundu siku hii.

Mpopi nyekundu umetumiwa kama ishara ya ukumbusho tangu Vita vya Dunia I

Jeshi la Ulinzi la Australia (Australian Defence Force) hivi karibuni limehusika katika mizozo huko East Timor, Iraki, Sudan na Afghanistan na imehusika katika opareshen za amani za Umoja wa Mataifa katika maeneo mengi ya ulimwengu, pamoja na Afrika, Mashariki Kati na eneo la Asia-Pasifiki.

Sir Edward ‘Weary’ Dunlop (1907 – 1993)

Sir Edward ‘Weary’ Dunlop alikuwa daktari mpasuaji mjasiri na wa kujali na shujaa wa Australia wa vita.

Wakati wa Vita vya Dunia II, Weary alikuwa daktari wa upasuaji wa Jeshi. Yeye na wanaume wenzake walishikwa na Wajapani na walipelekwa Burma kufanya kazi kwenye Reli ya Thai-Burma. Huu ulikuwa kazi ya muda mrefu na bidii.

Kama kamanda, Weary alitetea kwa wanaume wake na kama daktari wao wa upasuaji, alitumia masaa marefu kuwaponya. Aliteswa katika kambi lakini aliendelea kuhudumu.

Alituzwa mnamo 1969 kwa mchango wake kwa matibabu. Alipoaga dunia, watu 10 000 walijipanga katika mitaa ya Melbourne kwa mazishi ya kitaifa kwa shujaa waliyeita ‘Daktari wa Upasuajii wa Reli’ (The Surgeon of the Railway).

Uhamaji mnamo mapema 1900

Wakati kati ya Vita vya Dunia vya Kwanza na Pili, masharti ya vizuizi vya kuingia Australia yalibaki. Walakini, kulikuwa na kukua kwa watu wahamaji, haswa wanaume, kutoka Ulaya kusini. Walileta ustadi, elimu na thamani zao za kitamaduni. Walisaidia kukuza tasnia za Australia mashambani na kujenga barabara na reli. Wachonga mawe wenye ustadi walifanya mchango wa muhimu kwa ujenzi wa majengo yetu ya umma na ya makazi.

Mwishoni 1930, wakimbizi Wayahudi walianza kuwasili kutoka Ulaya. Walikuwa wanatoroka tishio la Nazi Ujerumani. Walitoka Ujerumani, Austria, Czechoslovakia, Hungary na Poland. Wengi wao walikuwa wamesoma na wakimbizi wenye vipawa ambao wangeweza kuchangia sana maisha ya utamaduni wa Australia.

Askari elfu kumi na saba wa Italia walioshikwa kwenye Vita vya Dunia vya Pili walizuiliwa katika jela za kambi za vita huko Australia. Walitendewa kwa haki. Walikaa tu kwa muda mfupi kwenye kambi lakini walijifunza kitu kuhusu nchi na watu wake. Baada ya vita, wengi walirudi Australia kama wahamiaji.

Mhamiaji wa Ulaya kuwasili huko Australia

Wakimbizi wa baada ya vita

Baada ya vita, Australia ilileta wahamiaji kutoka nchi zingine za Ulaya kujenga idadi ya watu. Mamilioni ya watu walikuwa wamekimbia Nazi Ujerumani au hawakuweza kurudi kwa nchi zao zilizomilikiwa na Urusi Soviet. Takriban 170 000 ya hawa watu waliofurushwa walikubaliwa kuingia Australia kuanza maisha mapya.

Kulikuwa na ukosefu mkali wa wafanyikazi huko Australia. Serikali ya Australia iliamini kwamba kukua kwa idadi ya watu ilikuwa muhimu kwa siku za usoni za nchi. Wahamiaji waliokomaa wenye afya nzuri chini ya umri wa 45 wangeweza kusafiri kwa £10 na watoto wao wangeweza kusafiri bure. Wanataifa, walakini, bado walizuia wale kuwa waliotoka Uingereza an Ulaya.

Kuchangamsha Australia, Serikali ya Australia ilianza kazi kwenye mpango thabiti mnamo 1949 kushikilia maji ya Mto wa Snowy kabla ya kufuata bahari huko Victoria mashariki. Maji haya yalibadilishwa njia kufuata nchi ya ndani kwa kunyunyuzia na kutumia kwa kuzalisha nguvu za umeme. Ulikuwa mradi mkubwa ulichukua miaka 25 kukamilisha. Asilimia sabini ya wafanyikazi kwenye mradi walikuwa wahamiaji.

The Snowy Mountains Hydro-Mpango wa Milima ya Snowy wa Uzalishaji nguvu za Umeme kutumia Maji

Mpango wa Milima ya Snowy ni ishara muhimu ya utambulisho wa Australia kama inayojitegemea, yenye tamaduni anuwai na nchi yenye rasilimali.

Ndio mradi mkubwa zaidi wa uhandisi huko Australia. Pia ni moja ya mpango mkubwa zaidi wa uzalishaji wa nguvu za umeme ulimwenguni.

Mpango unasambaza maji ambayo ni muhimu kwa tasnia za ukulima za nchi ya ndani huko New South Wales na Victoria. Vituo vyake vya umeme pia kuzalisha asilimia 10 ya umeme kwa New South Wales.

Asilimia 2 pekee ya Milima ya Snowy inaonekana juu ya ardhi. Ina mabwawa 16 kuu, vituo saba za umeme, na kituo cha pampu na njia za chini, mabomba na mifereji ya maji za kilomita 225.

Kazi kwenye mpango ilianza mnamo 1949 na ilimalizika mnamo 1974. Zaidi ya watu 10 000 kutoka nchi 30 walifanya kazi kwenye mradi. Asilimia sabini ya wafanyikazi hawa walikuwa wahamiaji. Baada ya mradi kukamilika, wafanyikazi wengi wa Ulaya walibaki kuishi huko Australia, walifanya mchango wa maana kwa jamii ya Australia yenye utamaduni anuwai.

Mpango wa Milima wa Snowy uko kwenye Mbuga la Kitaifa la Kosciuszko, New South Wales. Athari za mradi kwenye mazingira yameangaliwa kwa makini. Mpango ulimaanisha kwamba, katika baadhi ya maeneo, Mto wa Snowy sasa ulikuwa na asilimia 1 ya maji ambayo ulibeba hapo awali.

Kwa uzuri wa mazingira, serikali ya Victoria na New South Wales zimekubali kurejesha mwondo wa mto kwa asilimia 28.

Wafanyikazi kwenye Mpango wa Milima wa Snowy

Kutendewa kwa watu wa asili

Mnamo 1940 na 1950 sera ya Serikali ya Australia juu ya watu wa asili ilibadilika kuwa ya kuelewana. Hii ilimaanisha kwamba watu wa asili waliambiwa kuishi kama vile idadi ya watu wasio wa asili walivyoishi. Hii haikufanya kazi kwa sababu watu wa asili hawakutaka kupoteza desturi za utamaduni wao.

Mnamo 1960 sera ilibadilika kuwa umoja. Wanaume wengi wa Australia walipata haki ya kupiga kura mnamo 1850, lakini haki za Jumuiya ya madola za kupiga kura hazikuendelezwa kwa watu wa asili wa Australia hadi 1962. Umoja, watu wa asili walipewa uhuru wa kiraia lakini bado walitarajiwa kubadili utamaduni usio wa asili wa Australia.

Mabadiliko zaidi yalikuja mnamo 1967, wakati zaidi ya asilimia 90 ya Waaustralia walipiga kura ya 'NDIYO' kuruhusu watu wa asili kuhesabiwa kwenye sensa. Kura ya maoni ilikuwa hatua ya kihistoria. Ilionyesha kwamba umati mkubwa wa Waaustralia ulitaka watu wa asili kujumuishwa na kupewa haki sawa kama kila mtu mwingine.

Kufungua huku kwa nadhiria za Waaustralia, na upinzani mkali wa watu wa asili wakati huo, ulisababisha njia kwa sera ya watu wa asili walijitolea mnamo 1970. Serikali ya Australia ilikuja kutambua na kukubali kwamba Waaustralia wa asili wanapaswa kuweza kusema katika ukuzaji wao wa kisiasa, kichumu, kijamii na kitamaduni.

Uhamiaji – Badiliko la polepole

Mnamo 1950 na 1960, jamii ya Asia, makanisa na vikundi vya jamii pia vilipinga hadi mwisho wa sera ya 'Mwaustralia Mweupe'.

Mnamo 1958, Serikali ya Australia iliondoa jaribio la kusoma kwa nguvu na mnamo 1966 Australia ilifungua mlango kwa uhamaji wa wasio Waulaya na wenye ustadi wa Asia. Mwishowe Waaustralia kila mahali walitambua thamani ya kujumuisha mataifa yote katika mpango wao wa uhamaji. Sera ya 'Mwaustralia Mweupe' iliisha mnamo 1973, na nchi ilikuwa kwenye njia ya utamaduni anuwai.

Mnamo 1973, Serikali ya Australia iliondoa hitimu zote za rangi kwa uhamaji. Mnamo 1975, baada ya Vita vya Vietnamu, Australia ilikubali idadi kubwa ya wakimbizi na wahamiaji wa Asia.

Watu hawa walikuwa wanatoka Vietnamu lakini pia wahamiaji wa Uchina na India walianza kuwasili kwa idadi kubwa.

Kuanzia 1975, Australia imekubali wakimbizi kwa nchi nyingi za vita pamoja na Bosinia na Herzegovina, na kutoka kwa nchi katika Mashariki Kati na Afrika. Leo, wahamiaji wetu wanatoka kote ulimwenguni.

Australia imekuwa taifa la nchi zote; moja ya mafanikio kuu ya ulimwengu wa sasa. Kuanzia 1945, watu milioni 6.5 wamekuja Australia. Zaidi ya robo moja ya Waaustralia walizaliwa ng'ambo.

Wahamiaji wamechagua kuja Australia na kushiriki thamani zetu za pamoja. Wanaongezea ukubwa wa maisha ya Australia.

Ujumuishaji

Sasa Australia ni jamii yenye utamaduni anuwai ambapo haki ya kila mtu kufuata imani yake na desturi za kitamaduni katika sehemu ya sheria, inaheshimiwa na kulindwa.

Australia leo ina sera amilifu ya ujumuishaji, ambapo kila mtu wa rangi zote anahisi sehemu ya jamii. Sera inafanya kazi kwa sehemu zote za utamaduni wa Australia. Ni sehemu ya mtaala wa kielimu kuanzia utotoni kupitia chuo kikuu na ilifanywa na kazini mwetu na tasnia ya huduma.

Haki ya kila mtu ni kutendewa sawa bila ubaguzi na kulindwa na Tume ya Haki za Binadamu za Australia na vyombo vya serikali vya kuzuia ubaguzi katika kila jimbo na wilaya. Ubaguzi wa rangi unashutumiwa kwa umma na ni hatia chini ya sheria.

Australia imekuwa jamii ya utamaduni anuwai ya umoja na makubaliano. Ni nchi ambapo wahamiaji, watu wa asili na wengine waliozaliwa Australia wanaweza kujisikia huru kufuata malengo yao kwa amani. Ni mahali ambapo mizozo na chuki za zamani zinaweza kuachwa nyuma.

Dr Victor Chang (1936 – 1991)

Dr Victor Chang alikuwa mmoja wa wapasuaji bora wa moyo Australia.

Victor Peter Chang Yam Him alizaliwa Uchina mnamo 1936 na alikuja Australia wakati alikuwa miaka 15.

Alifanya kazi katika St. Vincent's Hospital ambapo mnamo 1984 waliunda kituo cha kwanza huko Australia katika upandikizaji wa moyo. Mnamo 1986, Dr Victor Chang alifanywa Mwenzi wa Mpangilio wa Australia (Companion of the Order of Australia), tuzo kubwa zaidi la Australia.

Vocyor alikuwa na hoja kuhusu ukosefu wa watoaji kwa hivyo aliazna kuunda moyo bandia, ambao ulikuwa karibu kukamilika wakati alipouawa kiyama mnamo 1991.

Kituo kipya cha utafiti kimeanzishwa kwa ukumbusho wake. Anakumbukwa kwa ujuzi wake, matumaini yake na uvumbuzi wake.

Albert Namatjira (1902 – 1959)

Albert Namatjira ni mmoja wa wasanii wakuu wa Australia ambao walioanzisha shule ya upakaji rangi ambayo inaendelea hadi waleo.

Kama kijana mchanga wa Arrernte, Albert alionyesha kibali cha asilia cha uchoraji.

Alikuwa na mafunzo kidogo ya uchoraji lakini michoro yake ya rangu ya maji ya nchi ya Australia yalikuwa maarifu sana na yaliuzwa haraka sana.

Yeye na mkewe walikuwa watu wa kwanza wa asilia huko Australia walioruhusiwa kuwa raia. Hii ilimaanisha wangeweza kupiga kura, kuingia hoteli au kujenga nyumba popote walipotaka. Albert raia wa Australia aliangaza ukweli kwamba watu was asilia hawakuwa ha haki hizi.

Maisha yake yalionyesha watu wasio wa asili wa Australia ukosefu wa haki ya sheria za ubaguzi wa rangi na walichangia kwa mabadiliko ya watu wa asilia.

Eddie Mabo (1936 – 1992)

Eddie Mabo alikuwa mwanaharakati na msemaji wa haki za nchi za asili.

Eddie Koiki Mabo alizaliwa huko Murray Island, kwenye nchi ya kitamaduni ya ukoo wa Mabo. Kuanzia umri mdogo, alifunzwa ni miti ipi haswa na miamba inawakilisha mipaka ya nchi ya familia.

Ilikuwa hadi miaka nyingi baadaye ambapo Eddie alijifunza kwamba nchi yake ilifikiriwa nchi kuu chini ya sheria ya Australia na haikuwa ya familia yake. Alirudisha hasira yake na kupeleka kesi yake kortini kwa hisani ya watu wa Murray Island.

Mnamo 1992, baada ya miaka nyingi, ksei ya Eddie ilishinda kwenye Mahakama Kuu. Uamuzi wa Mabo ulisema kwamba watu wa asili wangeweza kuthibitisha kwamba walikuwa historia na uhusiano wa kitamaduni unaoendelea kwa nchi yako, wangeweza kudai umiliki wa nchi ambayo haikuwa imedaiwa. Uamuzi huu umesababisha kurudi kwa maeneo kubwa ya wamiliki halisi.

Eddie Mabo anakumbukwa kwa ujasiri wake na kwa kupata haki za nchi kwa watu wa asili wa Australia.

Watu wa asili - miongo miwili ya mabadiliko

Watu wa asilia walipinga haki na walikuwa wameletwa kwa umma mnamo 1960 na mgomo wa Gurindji Strike kwa kituo cha ng'ombe huko Wave Hill Wilaya ya Kaskazini. Wachungaji wa asili, wakiongozwa na Vincent Lingiari, walitoka kazini katika kituo cha ng'ombe. Mgomo huu ulikuwa juu ya malipo na hali za kufanyia kzi, lakini ilibadilika kuwa amri ya haki za nchi. Matendo yao yalisababisha njia ambayo Eddie Mabo na wengine walipigania haki za nchi.

Chini ya *Sheria ya Haki za Nchi za watu wa asili (Wilaya ya Kaskazini) 1976* watu wa asili walipewa maeneo makubwa ya pori ya Australia. Mapema 1990, uamuzi wa Mahakama Kuu ya Mabo na Sheria ya *Cheo Wenyeji 1993 (Native Title Act 1993)* ilitambua watu wa asili walilazimika kudai nchi kwa msingi wa sheria na desturi zao za kitamaduni. Zaidi ya asilimia 10 ya nchi ya Australia sasa imechukuliwa na maamuzi ya wenyeji wa cheo. Hapa, sehemu za jamii ya kitamaduni bado inaendelea. Utamaduni wa asili unaendelea na unatambulika na jamii ya jumla.

Mnamo Mei 1997, ripoti ya 'Kuwaleta Nyumbani' iliwasilishwa katika Bunge la Australia. Ripoti ilikuwa kwa sababu ya swali la kuondolewa kwa idadi kubwa ya watoto wa watu wa asili na watu wa viziwa vya Torres Strait kutoka kwa familia zao. Watoto hawa walikuja kujulikana kama 'Vizazi Vilivyoibiwa'. Kwa sababu ya ripoti, maelfu ya Waaustralia walionyesha msaada wao kwa Waaustralia wenzao wa asili kwa kuandamana pamoja kwenye siku ya kwanza ya 'Siku ya Radhi' mnamo 1998.

Radhi kwa Vizazi Vulivyoibiwa, 2008

Mnamo 13 Februari 2008, Waziri Mkuu wa Australia aliomba radhi ya kitaifa kwa Vizazi Vilivyoibiwa katika Bunge la Australia. Alizungumza kwa niaba ya waustralia wote. Aliomba radhi kwa njia ambayo Waaustralia wa asili walikuwa wametendewa hapo zamani. Aliomba radhi haswa kwa njia ambayo watoto wa asili walikuwa wamechukuliwa kutoka wazazi wao.

Mazungumzo yaliwasilishwa kwenye stesheni za televisheni na redio. Maelfu ya Waaustralia hukusanyika pamoja kwenye maeneo na sehemu zao za kazi kusikiza hotuba ya 'Radhi'. Hotuba iliorodhesha ukosefu wa haki za zamani na waliomba radhi kwao. Hii ilikuwa hatua muhimu kwa kuponya watu wa asili na kuhakikisha kwamba ukosefu huu wa haki haitatendeka tena. Hotuba ya Radhi ilikuwa hatua muhimu ya mbele kwa Waaustralia wote.

Leo, mchango wa thamani wa watu wa asili kwa utambulisho wa Waaustralia kinatambulika na kusherehekewa. Watu wa asili na watu wa visiwa vya Torres Strait I walishikilia nafasi za juu kwa wafanyikazi wa kote Australia, pamoja na mfumo wa haki, siasa, sanaa na michezo. Mpango wa MARVIN, uvumbuzi wa watu wa asili katika katuni hai wa dijit,o umeshinda tuzo nyingi na unatumika katika taasisi za kielimu na kibiashara kwa zaidi ya nchi ishirini kote ulimwengu.

Mwandikishi wa angani anaandika 'Samahani' kule Sydney

Kwa kutamatisha

Kurasa hizi zimekupa tu mtazamo wa hadithi yetu ya Australia. Unaweza kupata kwamba haya ni maarifa mapya na yamefungua kujua kwako kwa mazingira yako. Unaweza kuanza kutazama tarehe kwenye majengo na kuziweka katika yaliyomo ya historia. Wakati unapopewa mpopi kuvaa mnamo 11 Novemba, utajua kwamba ni kukumbuka wanaume na wanawake wanajeshi walioanguka. Unapokutana na Waaustralia wa asili, utakuwa na hisia ya tamaduni za zamani na zinazowaongoza. Tunakuhimiza kupanua maarifa yako kwa kutumia rasilimali zetu za kawaida na kupitia kusafiri. Unavyojua zaidi, ndivyo utakavyogundua.

Tunakukaribisha kuwa raia wa Australia na tunakukaribisha kuhusika kikamilifu katika nchi yetu yenye amani na demokrasia.

Faharasa ya maswali yasiyoweza kujaribiwa

balozi
mtu anayewakilisha au kukuza nchi au shughuli

halmashauri
kundi la watu waliochaguliwa kufanya maamuzi, kwa mafano kuhusu jinsi kampuni inapaswa kuendeshwa

shule ya mabweni
shule ambayo wanafunzi huishi shuleni na hawarudi nyumbani kwa muhula wote wa shule

porini
mashambani Australia ambao bado ni hali asili

kituo cha ng'ombe
shamba kubwa ambalo ng'ombe huwekwa kwa uzalishaji wa nyama

hati
taarifa rasmi iliyoandikwa ya haki na majukumu

ukoo
kundi la watu, wanaohusiana kwa damu au ndoa, wanashiriki wilaya sawa

mwafaka
sehemu inayoshirikishwa ya kuzingatia

mwanajeshi mujibu wa sheria
mwanajeshi ambaye hakuchagua kujiunga na jeshi la ulinzi lakini alilazimika kujiunga wakati wa vita

Nchi ya Crown
nchi iliyokuwa ya serikali

mtaala
kozi ya masomo

fukara
kutokuwa na pesa au njia ya kupata pesa

didgeridoo
chombo cha muziki cha watu wa asili wa Australia iliyotengenezwa kutoka kwa mbao mrefu yenye shimo

bila mapendeleo
fursa ya maana na sawa kwa kila mtu kufanya vyema

mchezo usio na mapendeleo
kushiriki vyema katika juhudi ya kundi, kufuata sheria kwa faida ya kila mtu, kazi nzuri ya timu

wanajeshi wanaume na wanawake walioanguka
wanajeshi wanaume na wanawake waliouawa kwenye vita au mapigano

tengeneza
kujenga au kuunda

Bidhaa ya Jumla ya Nyumbani
thamani ya bidhaa na huduma zilizofanywa katika nchi kwa mwaka

wimbi la joto
hali joto sana ya anga inayodumu kwa zaidi ya siku mbili zikifuatana

uhaini mkubwa
hatia kali ya uhalifu ambayo inahusisha kujaribu kupindua serikali

michoro ya asili ya ikoni
sanaa ambayo ni ya kipekee na inaeleza watu wa asili

ukubwa wa ardhi
eneo la ardhi

hatua
tukio muhimu katika historia

cheo cha wenyeji
haki za kitamaduni ambazo watu wa asili wanazo kwa ardhi na maji, huamua katika mfumo wa sheria wa Australia

historia ya kuzungumza
makumbusho yanayozungumzwa na watu juu ya kilichotendeka zamani

mwanzilishi
mmoja wa wakazi wa kwanza, mfanisi katika siku za mapena za makazi ya kikoloni

uwakilishaji wa kisiasa
kuwakilishwa na mwanasiasa bungeni

hifadhi
eneo la nchi lililotengwa na serikali kwa watu wa asilia kuishi

kifungo
urefu wa wakati wa huduma za uhalifu kama adhabu

malipo yaliyowekwa
kuamua kiasi wafanyikazi wengi lazima walipwe kwa kazi yao

mabadiliko ya kijamii
kufanya mabadiliko kwa jamii pole pole, kuliko kwa mapinduzi

mazishi ya kitaifa
mazishi yaliyolipiwa na serikali kuheshimu raia ambaye amefanya mchango muhimu kwa taifa

boma
eneo liliozungukwa lilioundwa na miti ya mbao na vigingi

wachungaji
wanaume walioajiriwa kuchunga ng'ombe

mgomo
wakati wafanyikazi wameacha kufanya kazi, kwa mfano, kupinga uamuzi wa wafanyikazi

haki ya kupiga kura
haki ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa umma

kuapishwa
kukubaliwa kwa ofisi ya umma katika hafla ya rasmi

ratibishwa
kuwasiishwa rasmi kwa mjadala au idhini bungeni k.f ripoti ni thabiti

sehemu ya maisha
kitengo au asili ya kijamii, kazi, au nafasi

Kwa maelezo zaidi

Uraia wa Australia

Kupata maelezo zaidi juu ya jinsi ya kuwa raia wa Australia, tembelea tovuti ya uraia wa Australia katika www.citizenship.gov.au.

Australia

Unaweza kupata maelezo zaidi juu ya Australia katika maktaba ya eneo lako. Tovuti zifuatazo zinaweza pia kutoa maelezo zaidi:

- Maelezo muhimu za Australia www.dfat.gov.au/aib
- Lango la Utamaduni na Burudani www.cultureandrecreation.gov.au

Mipango na huduma za Serikali ya Australia

Unaweza kupata maelezo juu ya mipango na huduma za Serikali ya Australia kutoka kwa www.australia.gov.au.

Mbunge au Seneta wa Shirikisho

Mbunge wako wa shirikisho au Seneta wa jimbo au wilaya yako ana maelezo anuwai juu ya mipango na huduma za serikali ya Australia.

Orodha ya Wabunge na maseneta wanaweza kupatikana katika www.aph.gov.au.

Mashirika ya Serikali ya Australia

Unaweza kupata maelezo zaidi juu ya Mashirika ya Serikali ya Australia yaliyorejewa katika kitabu hiki cha msaada kutoka kwa tovuti zifuatazo:

- Australian Defence Force www.defence.gov.au
- Australian Electoral Commission www.aec.gov.au
- Australian Federal Police www.afp.gov.au
- Australian Human Rights Commission www.humanrights.gov.au
- Australian Sports Commission www.ausport.gov.au
- Australian Taxation Office www.ato.gov.au
- Australian War Memorial www.awm.gov.au
- Reserve Bank of Australia www.rba.gov.au

Mashirika yasiyo ya Serikali

Unaweza kupata maelezo zaidi juu ya Mashirika yasiyo ya Serikali ya Australia yaliyorejewa katika kitabu hiki cha msaada kutoka kwa tovuti zifuatazo:

- Bradman Foundation Australia — www.bradman.com.au
- Hamlin Fistula International — www.fistulatrust.org
- Royal Flying Doctor Service of Australia — www.flyingdoctor.net
- School of the Air — www.schoolair-p.schools.nsw.edu.au
- Snowy Mountains Hydro-Electric Authority — www.snowyhydro.com.au
- The Fred Hollows Foundation — www.hollows.org.au
- UNESCO World Heritage Centre — whc.unesco.org
- United Nations — www.un.org
- Victor Chang Cardiac Research Institute — www.victorchang.edu.au
- Volunteering Australia — www.volunteeringaustralia.org

Nyingine

Tafuta tovuti zifuatazo kwa maelezo zaidi juu ya mada zifuatazo:

- Katiba ya Australia — www.aph.gov.au/senate/general/constitution
- Tuzo za Mwaustralia wa Mwaka — www.australianoftheyear.org.au
- Ripoti ya 'Kuwaleta nyumbani' — www.humanrights.gov.au/social_justice/bth_report/index.html
- Hifadhi na mbuga za Jumuiya ya Madola — www.environment.gov.au/parks/index.html
- Waaustralia Maarufu: Kamusi ya Australia ya Wasifu wa Toleo la Mtandaoni — http://adbonline.anu.edu.au/adbonline.htm
- Orodha ya Miswada mbele ya Bunge — www.aph.gov.au/bills/index.htm
- Bunge la Australia — www.aph.gov.au
- Huduma za elimu za Bunge — www.peo.gov.au
- Sikukuu za Umma — www.australia.gov.au/topics/australian-facts-and figures/public-holidays
- Radhi kwa Vizazi Vilivyoibiwa, 2008 — www.abc.net.au/news/events/apology/text.htm

Shukrani

Picha zifuatazo zilitolewa kwa hisani ya Kumbukumbu za Kitaifa za Australia (National Archives of Australia):

uk42 - Watoto wa kituo cha kondoo NSW – Shule ya Angani, picha iliyochukuliwa mnamo 1962 (ref: A1200:L42511)

uk51 - Watu wenye sifa – Dick Smith, Mwenyekiti wa Civil Aviation Authority, 1991(ref: A6135:K23/5/91/1)

uk56 - Ramani ya Tasman ya Australia, 1644 (ref: A1200:L13381)

uk59 - Picha za Historia za mbio ya dhahabu huko Australia mnamo 1851 (ref: A1200:L84868)

uk60 - 'Afghans' na ngamia zao wakifanya kazi huko nchini Australia (ref:A6180:25/5/78/62)

uk67 - Watu wenye sifa - Sir Edward 'Weary' Dunlop katika ofisi yake, 1986 (ref: A6180:1/9/86/12)

uk67 - Uhamaji – Wahamiaji Waliowasili huko Australia – Wakata miwa wa Italia ngambi na Flaminia huko Cairns, 1955 (ref: A12111:1/1955/4/97)

Picha zifuatazo zilitolewa kwa hisani ya Maktaba za Kitaifa za Australia (National Library of Australia):

uk18 - Wapingaji walikutana kusikiza maspika kwenye Upinzani wa Vita uliofanywa huko Garema Place, Civic, Canberra, 15 Februari, 2003, picha na Greg Power (ref: nla.pic-vn3063592)

uk44 - Picha ya Judith Wright, ilichapishwa 1940s (ref: nla.pic-an29529596)

uk52 - Wanawake wa Indonesia wakisalimia wafanyikazi wa Jeshi la Ulinzi la Australia (Australian Defence Force) wakati wa operesheni ya msaada huko Aceh, Indonesia baada ya sunami, 30 Desemba 2004, picha na Dan Hunt (ref: nla.pic-vn3510861)

uk56 - Kundi la kwanza la Meli (First Fleet) huko Sydney Cove, 27 Januari, 1788, iliundwa na John Allcot 1888 – 1973 (ref: nla.pic-an7891482)

uk57 - Picha ya Caroline Chisholm, illichapishwa na Thomas Fairland 1804 – 1852 (ref: nla.pic-an9193363)

uk58 - Kurudi kwa Burke na Wills kwa Coopers Creek, iliundwa na Nicholas Chevalier 1828 – 1902 na kuchapishwa mnamo 1868 (ref: nla.pic-an2265463)

uk61 - Picha ya Catherine Helen Spence, ilichapishwa 1890s (ref: nla.pic-an14617296)

uk63 - John Simpson Kirkpatrick na punda wake, Gallipoli, 1915 (ref: nla.pic-an14617296)

uk65 - Picha ya Sir Charles Edward Kingsford Smith, ilichapishwa kati ya 1919 na 1927 (ref: nla.pic-vn3302805)

uk70 - Picha ya Albert Namatjira huko Hermannsburg Mission, Wilaya ya Kaskazini (Northern Territory), ilichapishwa 1946 or 1947 naArthur Groom (ref: nla.pic-an23165034)

Maneo ya Urithi wa Kumi na nne wa Ulimwengu yalitolewa kwa niaba ya Idara ya Mazingira, Maji, rithi na Sanaa na watu wafuatao:

uk40 - Maeneo ya Visukuku vya Wanyama wa Australia picha na Colin Totterdell

uk40 - Mbuga la Kitaifa la Blue Mountains picha na Mark Mohell

uk40 - Kisiwa cha Fraser picha na Shannon Muir

uk40 - Msitu wa Mvua wa Gondwana wa Australia picha na Paul Candlin

uk40 - Mbuga la Kitaifa la Kakadu picha na Sally Greenaway

uk40 - Kisiwa cha Lord Howe picha na Melinda Brouwer

uk40 - Kisiwa cha Macquarie picha na Melinda Brouwer

uk41 - Mbuga la Kitaifa la Purnululu picha na Purnululu picha na Rod Hartvigsen

uk41 - Jumba la Maonyesho ya Kifalme na Bustani za Carlton picha na Michelle McAulay

uk41 - Shark Bay picha na Kelly Mullen

uk41 - Nyika la Tasmania picha na Nicola Bryden

uk41 - Mbuga la Kitaifa la Uluru-Kata Tjuta picha na Andrew Hutchinson

uk41 - Tropiki zenye maji za Queensland picha na Colin Totterdell

uk41 - Maeneo ya Maziwa ya Willandra picha na Mark Mohell

Picha zifuatazo zilitolewa kwa hisani ya iStockphoto:

Ukurasa wa Mbele - Ufito, ©iStockphoto.com/Ressy (ref: 3322510)

uk14 - Opali nyeusi ya Australia, ©iStockphoto.com/Alicat (ref: 8323912)

uk22 - Jumba la Bunge, ©iStockphoto.com/Tim Starkey (ref: 2256743)

uk22 - Nyundo ya dalili na kitabu, ©iStockphoto.com/Dem10 (ref: 2397687)

uk27 - Sarafu kwenye grafu ya fedha, ©iStockphoto.com/Robyn Mackenzie (ref: 2335549)

uk27 - Uandishi wa Daktari, ©iStockphoto.com/Carlos Arranz (ref: 6498434)

uk38 - Ufuo wa Bondi, ©iStockphoto.com/Edd Westmacott (ref: 3048786)

uk38 - Kings Canyon, ©iStockphoto.com/Francois Marclay (rejeo: 5733853)

uk51 - Uchukuaji wa eneo la mbale ya chuma, ©iStockphoto.com/Christian Uhrig (ref: 9819736)

uk54 - Digeridoos, ©iStockphoto.com/Adam Booth (ref: 834207)

uk55 - Sanaa ya mawe ya watu wa asili – samaki ya Saratoga, ©iStockphoto.com/Alpen Gluehen (ref: 2761924)

Picha zingine zote zilitolewa kwa hisani ya mashirika/watu wafuatao:

uk8 - Gamu zilizoonekana na vifuniko ya chini Burrawang palms, Mbuga la Kitaifa la Murramarang, NSW, picha na Dario Postai

uk20 - Mtu akiweka kura yake kwenye sanduku za kupigia kura kwa hisani ya Tume ya Uchaguzi ya Victoria

uk24 - Sheria ya Katiba ya Jumuiya ya Madola ya Australia 1900: Rekodi Halisi ya Umma, picha kwa hisani ya Zawadi Ukusanyaji, Sheria ya Sanaa ya Jumba la Bunge, Idara ya Huduma za Bunge, Canberra ACT

uk27 - Watoto wamekaa kwa safu picha kwa hisani ya Getty Images, picha na Mel Yates

uk28 - Mahakama Kuu picha kwa hisani ya Mahakama Kuu ya Australia

uk40 - Kisiwa cha Big Ben Heard picha kwa hisani ya Australian Antarctic Division © Commonwealth of Australia, picha na L. E. Large (ref:1892A2)

uk40 - Great Barrier Reef picha kwa hisani ya Great Barrier Reef Marine Park Authority

uk41 - Jumba la Sydney Opera picha kwa hisani ya Jiji la Sydney, picha na Patrick Bingham-Hall

Shukrani

uk43 - Mwanachama wa timu kutoka kwa timu ya taifa ya kandanda ya wanawake (Matildas) picha kwa hisani ya Tume ya Michezo ya Australia

uk44 - Sir Donald Bradman picha kwa hisani ya Jumba la Kumbukumbu la Kriketi la Bradman. Sir Donald Bradman akiwa amevaa Kofia ya Jaribio la Australia wakati wa msimu wa Australia wa 1931-32

uk45 - Professa Fred Hollows picha kwa hisani ya Mfuko wa Fred Hollows, picha na Frank Violi

uk50 - Fataki za kuamkia Mwaka Mpya juu ya Sydney Harbour picha kwa hisani ya Jiji la Sydney

uk52 - Dr Catherine Hamlin AC picha kwa hisani ya Mfuko wa Hamlin Fistula Relief na Msaada

uk61 - Lord Lamington anahotubia umati wa Siku ya Shirikisho, Brisbane, 1901, picha kwa hisani ya Maktaba ya Jimbo la Queensland, picha na H.W. Mobsby (ref: 47417)

uk65 - Jikoni ya Supu picha kwa hisani ya Maktaba ya Jimbo la New South Wales (Mitchell Library). Watoto wa shule hupanga laini kwa toleo la bure la supu na kipande cha mkate, Shule ya Umma ya Belmore Kaskazini NSW, 2 Agosti 1934, picha na Sam Hood (ref: H&A 4368)

uk66 - Njia ya Kokoda picha kwa hisani ya Ukumbusho wa Vita vya Australia (ref: 014028)

uk66 - Mpopi nyekundu katika Ukumbusho wa Vita vya Australia, picha na Torie Brims

uk70 - Dr Victor Chang picha kwa hisani yaTaasisi ya Utafiti wa Moyo ya Victor Chang

uk70 - Eddie Mabo picha ilitolewa tena na ruhusa ya Bernita na Gail Mabo